# Nipashe

Jumatano Desemba 15, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580430

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




Nipashe

TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • BURUDANI

RPC, hakimu ni majemedari wapya mapambano shuleni

ELIMU NA MWALIMISHI WETU

SIMULIZI...

Ndivyo 'tochi' ilivyompa mwanafunzi ulemavu

UKURASA 11

**Serikali** yaahidi bei elekezi ya maziwa

UKURASA 3



**Mshtakiwa** aachiwa kesi mauaji ya Mawazo

UKURASA 3

# 14 wafa ajalini

• **Ni** ndugu, marafiki waliokuwa wanatoka harusini, baada ya lori na Hiace kugongana, JPM atuma salamu... *Endelea ukurasa 4*

## YALIYOMO


UKURASA WA 7

**MWANAFUNZI WA KIKE KINARA KWA UFAULU ARU AFUNGUKA**

MWANAFUNZI wa kike, Jasmine Mndeme (23), aliyeibuka mwanafunzi bora zaidi kati ya wehitimu 926 wa...

UKURASA WA 8

**BITEKO AFUTA LESENI 7, ASIMAMISHA KAZI 3**

SAKATA la utoroshaji wa madini wilayani Chunya, mkoani Mbeya, limechukua sura mpya baada ya...


## Kina Mdee wafunguka kuhusiana rufani yao



UKURASA 2



Baadhi ya washtakiwa 13 wakiwamo vigogo wanane wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), wakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: HELLEN MWANGO**

# Vigogo BoT kortini madai kuharibu noti za bil. 4.6/-


**MICHEZO** UEFA YAMRUDISHA NEYMAR BARCELONA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Mwanafunzi shule ya awali Feza, Bijan khorshi Hassan, akimkabidhi risala kwa mgeni rasmi Mh. Ezra Chilewesa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo, baada ya kuisoma kwenye mafahali hayo. Kulia ni Mustafa Ceric, Mkuu wa Shule ya Msingi Feza na Mkuu wa Shule ya Feza ya Awali, Arzu Yilmaz. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vigogo 8 BoT kortini madai kuharibu noti za bilioni 4.6/-

**Na Hellen Mwango**

WATU 13 wakiwamo vigogo wanane wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, wakikabiliwa na mashtaka ya kuharibu noti za Sh. 10,000 zenye thamani ya Sh. 460,000 na kuisababishia benki hiyo hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 4.6.

Vigogo hao wa BoT ni, Mariagoretha Kuzugala, Henry Mbowe, Asha Sekiboko, Cecilia Mpande, Agripina Komba, Zubeda Mjewa, Khadija Kassunsumo na Mwanakheir Omary.

Washtakiwa wengine ni, Alistides Genand, Shukuru Mchegage, Musa Chengula, Zaituni Chihipo na Respicius Ishengoma, wote kwa pamoja walisomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Godfrey Isaya.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, akisaidiana na Mawakili wa Serikali Waandamizi, Wankyo Simon, Turumanya Majigo na Jaqline Nyantori.

Nyantori alidai kuwa kati ya Januari mwaka 2017 na Septemba 30, 2019, watumishi hao kwa kuvunja majukumu yao ya kazi waliwezesha utendekaji wa kosa la kuongoza genge la uhalifu.

Katika shitaka la pili, ilidaiwa kuwa, katika tarehe hizo na maeneo hayo, jijini Dar es Salaam, washtakiwa Genand, Mchegage, Chengula, Chihipo na Ishengoma wakiwa si watumishi wa BoT, kwa kushirikiana na watumishi hao wa BoT kwa makusudi, waliwezesha kutendeka kosa la uhalifu wa kupanga.

Katika shitaka la tatu, ilidaiwa kwamba, katika tarehe hizo jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote bila ya kuwa na kibali na kutokuwa wazalendo, waliharibu kwa kukata noti 460,000 za Sh. 10,000 sawa na Sh. bilioni 4.6.

Majigo alidai kuwa, katika tarehe tofauti, jijini Dar es Salaam, kwa mawasilisho ya kilaghai, kwa kujua na kwa mpango wa kitapeli washtakiwa wote walijipatia faida ya Sh. bilioni 1.5 kutoka BoT baada ya kuwasilisha noti hizo.

Shtaka la tano ilidaiwa kuwa watumishi hao wa BoT na wenzao walitakatisha fedha kwa kujihusisha na miamala tofauti ya Sh. bilioni 1.5, wakati wakijua zilitokana na kosa tangulizi la uhalifu wa kupangwa na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Katika shtaka la sita, washtakiwa wote katika tarehe hizo jijini Dar es Salaam, waliisababishia BoT hasara ya Sh. bilioni 4.6.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, washtakiwa walielezwa kwamba, mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi hivyo watapelekwa mahabusu hadi upelelezi utakapokamilika.

Wakili Kadushi alidai, upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Isaya alisema kesi hiyo itatajwa Desemba 28, mwaka huu na washtakiwa wapelekwe mahabusu.

# Wabunge CHADEMA: Muda wa kukata rufani bado upo

**Na Elizabeth Zaya**

WABUNGE 19 akiwamo aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chama hicho (BAWACHA), Halima Mdee, wamesema bado wana muda wa kukata rufani ya kupinga kuvuliwa uanachama kama walivyopanga.

Kauli hiyo ilitolewa jana na aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo, Hawa Mwaifunga, ambaye naye amevuliwa nyazifa hiyo pamoja na uanachama, wakati akizungumza na Nipashe.

"Bado muda upo tutakata tu rufani kama tulivyosema pale kwenye mkutano na waandishi wa habari,"alisema Mwaifunga.

Desemba Mosi, wakizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, wabunge hao, walidai kwamba wangekata rufani ya kuvuliwa uanachama kwa Baraza Kuu la Chama baada ya kushauriana na wanasheria wao.

Wakiwa katika mkutano huo na waandishi wa habari, walidai kupokea barua hiyo jana yake kabla ya siku hiyo ya mkutano.

Katika mkutano huo, Mdee alisema ndani ya siku 30, baada ya kutafakari na kushauriana na wanasheria wao watakuwa wamekata rufani hiyo kwa Baraza Kuu la chama hicho huku akidai kwamba kwa kipindi hicho chote ambacho watakuwa wakisubiri uamuzi wa rufani wataendelea kuwa wanachama wa hiari na ving`ang`anizi kutokana na mapenzi waliyonayo kwa chama chao.

"Kamati Kuu imefanya uamuzi wake, tumekuja hapa tunasema tunaenda kukata rufaa Baraza Kuu, sasa kisheria siwezi kujadili hapa nje content ya kile ambacho tutakwenda kujadili na mamlaka za juu ya chama, suluhu siyo kuja hapa na kuanza kusema, uamuzi umeshafanyika na tumepewa adhabu lakini na sisi tunaenda kukata rufani kwenye kikao kikubwa," alisema Mdee wakati akizungumza na vyombo vya habari Desemba Mosi, mwaka huu.

Aliongeza: "Na sheria inasema huwezi kuanza kuzungumza msingi wa kesi kwenye chombo cha habari kabla hujaenda kwenye mamlaka yenyewe ambayo inatakiwa kukusikiliza. Sitazungumza hapa chanzo cha sisi kwenda bungeni, ila ipo siku nitazungumza."

Desemba 3, akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, alisema kwamba kwa mujibu wa Katiba ya chama chao, wanatakiwa kukata rufani ndani ya siku 30 tangu kuvuliwa uanachama ambapo mpaka tarehe hiyo walikuwa hawajakata rufani hiyo.

Hata hivyo, juzi Mrema alipoulizwa kama chama kimepokea rufani hiyo kutoka kwa wabunge hao, alimtaka mwandishi ampigie baadaye.

Lakini mwandishi alipompigia, Lema hakupokea hadi tunakwenda mitamboni.

CHADEMA ilifikia hatua ya kuwavua uanachama wanachama wake 19 baada ya kukiuka msimamo wa chama chao wa kutovitambua kutokana na kutokubaliana na matokeo ya uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu.

Wabunge hao wanadaiwa kukaidi msimamo wa chama na kuamua kwenda kuapishwa bungeni bila barala za chama, ambapo pia kinasema hakikupeleka majina yao kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuthibitisha kuwa ni wabunge wake halali.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapt (Mst) George Mkuchika, akimkabidhi nyaraka za kiutumishi Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi mara baada ya viongozi hao kuripoti rasmi leo ofisini na kuanza kazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mshtakiwa aachiwa huru kesi mauaji ya Mawazo

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, imemuachia huru mshtakiwa wa wanne katika kesi ya mauaji ya aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wa mkoa huo, ambaye pia alikuwa mgombea unungе Jimbo la Busanda mwaka 2015, Alphonce Mawazo.

Mshtakiwa huyo, Habibu Feruzi, aliachiwa huru jana, baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wake, huku washtakiwa wanne wakikutwa wana kesi ya kujibu.

Mahakama hiyo ilimuachia huru mshtakiwa Feruzi kutokana na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri dhidi yake kuwa dhaifu.

Baada ya kukutwa na kesi ya kujibu, watuhumiwa hao wanatakiwa watoe utetezi wao kwenye kesi hiyo namba 9/2019.

Washtakiwa hao ni Alfan Apolinari (41), Epafula Zacharia (39), Hashimu Sharifu (45) na Kululinda Bwire (31) wote wakazi wa Katoro mkoani Geita.

Washtakiwa hao walifikishwa katika Mahakamani ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita jana majira ya saa 2:30 asubuhi na kupandishwa kizimbani majira ya saa 3:15 asubuhi mbele ya Naibu Msajiri Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza ambaye ni Hakimu Mkazi Mwandamizi Mwenye Mamlaka ya Ziada, Frank Mahimbali, na walipaosomewa shtaka lao la mauaji walikana.

Hakimu Mahimbali akitoa uamuzi huo mdogo, alisema kwa mujibu wa ushahidi uliyotolewa na upande wa Jamhuri umewagusa washtakiwa wote.

Hata hivyo, alisema ushahidi dhidi ya mshtakiwa wa wanne Feruzi ni dhaifu, hivyo mahakama inamuachia huru, lakini washtakiwa wanne waliobaki wamekutwa na kesi ya kujibu na wanatakiwa kutoa utetezi wao.

Upande wa utetezi ukiongozwa na mawakili wa watano kila mmoja akimtetea mshtakiwa mmoja ni Yisambi Siwale, Flora Enosy, Laurent Bugoti, Abel Sizya na Paul Hombo.

Walidai kuwa mshtakiwa wa kwanza, Alfan Apolinari, atajitetea kwa kiapo na atakuwa na mashahidi wawili na kielelezo kimoja.

Mshtakiwa wa pili, Epafula Zacharia, atajitetea kwa kiapo na atakuwa na mashahidi wawili na kielelezo kimoja wakati mshtakiwa wa tatu Hashimu Sharifu atajitetea kwa kiapo yeye mwenyewe wala hatakuwa na shahidi wala kielelezo.

Mshtakiwa wa tano, Kululinda Bwire, atajitetea kwa kiapo na atakuwa na mashahidi wawili na kielelezo kimoja.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mawakili watatu Javelin Rugaihuruza, ambaye ni Wakili wa Serikali Mkuu, Hezron Mwasimba ambaye ni Wakili wa Serikali Mwandamizi na James Pallangyo ambaye ni wakili wa serikali wote waliieleza Mhakama kuwa upande wa Jamhuri umefunga ushahidi wao wa mashahidi 13 na vielelezo nane.

Baada ya kutoa uamuzi huo, Hakimu Mahimbali aliahirisha kesi hiyo kwa ajili ya upande wa utetezi kuanza kutoa ushahidi jana jioni.

Tangu kesi hiyo ianze kusikilizwa, mashahidi 13 wa Jamhuri walitoa ushahidi wao wakiwa na vielelezo nane.

Awali akisoma hati ya mashtaka Msaidizi wa Kumbukumbu Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, Martina Nelei, alidai kuwa Novemba 14, mwaka 2015 katika Kijiji cha Rudete Mkoa wa Geita, washtakiwa wote kwa pamoja walimuua Alphonce Mawazo, kitendo ambacho ni kinyume cha kifungu 196 na 197 cha sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

## Serikali kutoa bei elekezi maziwa

**Na Lulu George,** TANGA

SERIKALI imeahidi kuharakisha utoaji wa bei elekezi ya maziwa ili wafugaji wanufaike tofauti na sasa.

Pia, imesema kuna mikakati ya kuongeza thamani ya zao hilo ili kuleta ushindani wa ubora katika soko la ndani na nje ya nchi.

Ahadi hiyo ilitolewa na Naibu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini, Charles Malunde, katika mahojiano na Nipashe, baada ya kikao kazi kilichoshirikisha vyama vya msingi vya ushirika mkoani humo kwa uratibu wa Chama Kikuu cha ushirika wa wafugaji mkoani Tanga (TDCU).

Aliwataka wafugaji kuachana na ufugaji wa mazoea na kufanya wa kisasa ambao utakuwa na tija kwa maendeleo yao binafsi na kwa maslahi ya taifa.

Bei ya maziwa mkoani Tanga ni Sh. 1,200 kwa lita moja huku pakiti moja yenye ujazo wa milimita 250 (sawa na robo lita) yanayotoka viwandani yakiuzwa kwa Sh. 600.

Malunde alisema licha ya bei iliyopo kulalamikiwa na wafugaji wengi, inaweza kumpa faida ndogo hasa kwa mfugaji ambaye atatumia mbinu bora na za kisasa za kilimo ikiwamo kuongeza lishe, mitamba yenye ubora na kuhakikisha anaongeza uzalishaji wa maziwa kila siku.

"Katika hili lazima tuelewane, haiwezekani mfugaji huwalishi ng'ombe wako kama inavyotakiwa, unazalisha lita tati za maziwa kwa siku, mitamba yenyewe unachukua ya mtaani tu halafu utegemee maziwa yakupe faida hilo litakuwa ndoto," alisema.

"Hata kama serikali itapandisha bei ya maziwa, lakini hutaweza kutumia bidhaa hiyo kujiletea maendeleo utaona kwamba biashara haina faida," alisema.

Alisema upo mpango uliowekwa kwa wafugaji kupitia vyama vyao vikuu vya ushirika kuwakopesha mitamba bora ya kisasa kwa utaratibu wa kukusanya kiwango fulani cha maziwa kila siku kama malipo ya mitamba hiyo watakopa.

"Kuna utaratibu umewekwa kupitia vyama vikuu vya ushirika ambapo mfugaji ataweza kupeleka maziwa lita tano kila siku, ikiwa ni fidia ya malipo ya mkopo wa mtamba atakaokopeshwa kwa mujibu wa makubaliano watakayowekeana hivyo wafugaji wachangamikie fursa hiyo," alifafanua.



# Watu 14 wafariki dunia kwenye ajali

**Na Mwandishi Wetu**

WATU 14 wakiwamo ndugu na marafiki waliokuwa wanatoka harusini mkoani Mwanza kwenda Itigi, wilayani Manyoni, mkoani Singida, wamefariki dunia papo hapo katika ajali iliyosababishwa na Hiace na lori la mafuta kugongana uso kwa uso.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Sweetbert Njewike, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo Desemba 12, mwaka huu, majira ya saa 9.30 alasiri.

Kutokana na ajali hiyo, Rais John Magufuli, ametuma salamu za pole kwa familia za watu waliopatwa na msiba wa kuondokewa na ndugu zao hao 14 wilayani Ikungi, mkoani Singida, juzi jioni.

Kamanda Njewike alisema, ajali hiyo ilitokea baada ya gari dogo aina ya Hiace lililokuwa likitoka Mwanza kwenye harusi likienda Itigi, kulipita gari jingine bila kuchukua tahadhari na kugongana uso kwa uso na lori la mafuta.

Dereva wa Hiace ni miongoni mwa watu waliofariki dunia katika ajali hiyo.

Wengine waliokufa katika gari hilo ni ndugu wakiwamo binadmu, shangazi, mjomba na kwamba majina yao hayajatambulika.

Kamanda alisema jali hiyo ilitokea katika kijiji cha Mkiwa, wilayani Ikungi, barabara kuu ya Singida baada hiace hiyo kugongana uso kwa uso na lori la mafuta lililokuwa likitoka Dar es Salaama kwenda Kahama, mkoani Shinyanga.

Katika ajali hiyo watu 14 walikufa papo hapo na watatu walijeruhiwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, Rais Magufuli alimtaka Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, kufikisha salamu za pole kwa wafiwa wote.

"Nawapa pole wafiwa wote, Mwenyezi Mungu awatie nguvu, uvumilivu na ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu cha kuondokewa na wapendwa wenu, nawaombea marehemu wote wapumzike mahali pema peponi na majeruhi wote wapone haraka," alisema.

Rais Magufuli, alivitaka vyombo vinavyosimamia usalama wa barabarani kuongeza jitihada za kudhibiti ajali hasa katika kipindi hiki cha kufunga mwaka, ambacho kumekuwa kukitokea ajali nyingi za barabarani.

Pia, Rais Magufuli amewataka watumia barabara zote kuwa makini na kujiepusha kuvunja sheria na taratibu za barabarani.



Wafanyakazi wa kampuni ya ujenzi ya Eima General Supplies ya mjini Songea, wakifanya ukarabati wa barabara ya Mpate, iliyopo katikati ya Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma jana. **PICHA: MICHAEL EMMANUEL**

## Wabunge wa wanne ACT kuapa wiki hii

**Na Elizabeth Zaya**

WABUNGE wanne wa Chama cha ACT-Wazalendo wanatarajia kutinga bungeni kuapa wakati wowote ndani ya wiki hii.

Wabunge hao ni Salum Mohamed Shafi, Halifa Mohamed Issa, Omary Ali Omary, na Khatibu Said Haji, wote kutoka Zanzibar.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama hicho, Ado Shaibu, alisema chama hicho kimeamua kuwaruhusu wabunge na wawakilishi wa chama hicho kwenda bungeni kwa kusimamia hoja za msingi ambazo zitaleta mabadiliko.

"Wabunge wetu tumeshawapa baraka zote za kwenda bungeni wakati wowote kuanzia sasa, tumeona tuwaruhusu waende lakini kwa kuhakikisha wanakwenda na hoja ambazo zitaleta changamoto, hawaendi kujibweteka na kufikia uamuzi huu kulifanyika majadiliano ya muda mrefu," alisema Shaibu.

"Tunakumbuka tulikuwa na mbunge mmoja katika bunge lililopita, Zitto Kabwe, lakini alikuwa na hoja ambazo zilikuwa zikiamusha bunge kana kwamba wako wengi, tunaamini kwamba pamoja na yote yaliyotokea, na chama kufikia uamuzi huo, wabunge hao wanaokwenda watakwenda kuwakilisha vema, hatutaki wawe ni wabunge wa kwenda kutulia tu huko."

Hivi karibuni akiwa bungeni, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliwataka wabunge hao kwenda bungeni kuapa ili wapangiwe kazi za kufanya.

Ndugai alisema hakuna sababu kwa wabunge wa chama hicho kuendelea kuzurula mtaani kama waliomba kuwatumikia wananchi wao.

Chama hicho tayari kimeridhia ombi la serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar la kujenga serikali ya umoja wa Kitaifa na Maalim Seif Sharif Hammad kutoka chama cha ACT-Wazalendo ndiye Makamu wa kwanza wa serikali hiyo ya awamu ya nane.

# Serikali yahamasisha wananchi kujiunga CHF

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeanzisha kampeni ya kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) uliyoboreshwa kupitia vyombo vya habari, ili kuongeza idadi ya wanachama.

Hastua hiyo imetokana na kusuasua kujiandikisha kwani hadi sasa ni watu milioni 3.3 tu ndiyo waliojiandikisha.

Mkurugenzi wa Afya,Ustawi wa Jamii na Lishe Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Ntuli Kapologwe, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema lengo la kampeni hiyo ni kuhamaisisha wananchi kujiunga na mfuko huo ili wanapougua wapate matibabu hata kama watakuwa hawana fedha mkononi.

"Tafiti zinaonyesha kuwa watu wengi wasio kuwa na bima wanapata shida wanapohitaji huduma za afya kwa kukosa pesa za papo kwa papo, lakini mfuko huu utawawezesha kupata matibabu katika hospitali yoyote ya serikali eneo lolote nchini," alisema Dk. Kapologwe.

Alisema kampeni hiyo itatekelezwa kutokana na serikali kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya afya kwa kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na kuboresha miundombinu pamoja na vifaa tiba, hivyo ni lazima watu wajiunge katika mfuko huo ili kupata matibabu ya uhakika.

"Tunataka idadi kubwa ya wanachi wajiunge ili vituo hivi vya afya viweze kujitegemea na kujiendesha vyenyewe kutokana na michango ya wananchi, na serikali pia inajazia kiasi Fulani," alieleza.

Alisema serikali kwenye mfuko huo imechangia Sh. bilioni 2.3 na wananchi wamechangia Sh. bilioni 14.

Alisema bado uhitaji wa wananchi kujinga na mfuko huo ni mkubwa sana, kwa kuwa takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 86 ya wananchi hawajajiunga na mfuko wowote wa bima ya afya.

"Lakini pia hadi hivi sasa uchangiaji katika mfuko huu ni asilimia tano, na kaya zilizojiunga ni 557,000 bado ipo haja wananchi kujiunga kwani mfuko huu ndiyo mkombozi wao katika masuala ya matibabu... tunataka hadi mwakani mwezi kama huu tufike asilimia 20 ya uchangiaji," alisema.

Pia, alisema mfuko umefanyiwa maboresho mengi ikiwamo kuongeza mafao kama fao la upasuaji mdogo na mkubwa, huduma za mionzi, tiba ya mazoezi kwa waliopata kiharusi na rufani hadi hospitali kubwa nchini.

Kadhalika, alisema kuwa kupitia utafiti, watu wengi walipendekeza kaya ya watu sita ilipe Sh.30,000 kwa mwaka na kwa jiji la Dar es Saalam kaya yenye watu sita ni Sh. 150,000.

Dk. Kapologwe aliwaagiza waganga wakuu wa wilaya kuhakikisha wanasimamia utoaji wa huduma za afya ikiwamo kutoa elimu ya umuhimu wa kujiunga na mifuko ya bima ya afya.

HABARI KITAIFA

# Aweso atimua kazi watatu DDCA

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amewatimua kazi wafanyakazi watatu wa Wakala wa Uchimbaji Visima (DDCA), kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao.

Watendaji walioondolewa ni Mkuu wa Kitengo cha Utafiti wa Maji Ardhini, Fadhil Sauko, Mkuu wa Kitengo cha Ufundi, Abdallah Abdulrahman na Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi, Hamad Msuya.

Waziri Aweso alichukua hatua hiyo jana wakati wa ziara yake Wilaya ya Mkuranga kukagua miradi ya maji inayosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

Aweso alisema wafanyakazi waliotimuliwa watapangiwa majukumu mengine kutokana na kushindwa kutekeleza wajibu wao.

"Nimewaondoa hawa watendaji wasubirie kupangiwa majukumu mengine, hatuwezi kuwa na watu ambao wanashindwa kutekeleza majukumu ya serikali ya kuhakikisha wanapeleka maji kwa wananchi," alisema Aweso.

Alisema serikali ilianzisha DDCA kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata maji, matokeo yake kumefanyika hujuma kwa watendaji.

Aidha, alisema kitengo cha utafiti wa maji kilipewa magari manne na yote yameharibika na kuhitajika mengine mapya.

"Serikali ilitoa magari manne kwa sasa yote yamekufa ukiangalia ya mkuu wa kitengo hicho cha utafiti wa maji magari yake yanafanyakazi," alisema Waziri Aweso.

Aliiagiza DAWASA kuongeza mikoa ya huduma ya maji Dar es Salaam ili kuwafikia wananchi wa pembezoni ambao hawapati huduma hiyo ikilinganishwa na wanaoishi katikati ya mji.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Cyprian Luhemeja, alisema katika utekelezaji wa miradi ina changamoto ikiwamo umwagilijia wa zege kuwa mgumu kipindi cha mvua na kusababisha kazi iendelee kusuasua.

"Zege iliyoletwa haikidhi viwango hivyo kusababisha mkandarasi abomoe ili aanze upya kwa uhakiki zaidi baada ya kubadilisha utaratibu wa uchanganyaji wa zege badala ya kuletwa na wakala alichanganya site siku ya kazi," alisema.

Alisema ugonjwa wa Covid-19 ulisumbua hasa upunguzaji wafanyakazi licha ya kazi kuendelea kwa utaratibu maalum.

## Prof. Janabi ashauri Watanzania kupima afya

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wameshauriwa kupima afya zao mara kwa mara na kufanya mazoezi ili kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza ambayo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka hasa kisukari na shinikizo la damu.

Ushauri huo ulitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Profesa Mohamed Janabi, wakati wa jumuiko la wanataaluma katika Chuo Kikuu Ardhi (ARU) lililofanyika chuoni hapo.

Magonjwa yasiyo ya kuambukiza yanayoelezwa kuongezeka duniani na kusababisha vifo vingi ni saratani, figo, kisukari na shinikizo la damu.

Profesa Janabi alisema magonjwa yasiyoambukiza ni tishio na yanazidi kuongezeka na kwamba kuna umuhimu mkubwa kwa wananchi kuchukua tahadhari za kiafya ikiwamo kupima na kujua hali ya afya zao.

"Magonjwa haya yanayongezeka duniani sasa tunapopata fursa kama hii kuelezea magonjwa yasiyo ya kuambukiza tunawasisitiza wananchi hatua za kuchukua ili kujikinga kabla ya kupata maradhi hayo," alisema Profesa Janabi ambaye ni bingwa wa maradhi ya moyo.

Alisema watu wanapaswa kuwa waangalifu kwenye matumizi ya dawa kwa kuwa wanapaswa kutumia kwa ushauri wa madaktari badala ya kutumia holela.

"Wagonjwa wa moyo ambao wameshagundulika wanywe dawa kama walivyoshauriwa na madaktari na ambao hawajapima wakapime ili wajiweke kwenye nafasi nzuri badala ya kukaa tu bila kujua hali yako," alisema.




# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Utashi wa kisiasa utaliponya taifa

**UTASHI** wa kisiasa umeonyesha mafanikio makubwa katika kulinda maliasili ya taifa ambayo imeliingizia taifa mamilioni ya fedha ikiwamo za kigeni.

Miaka ya nyuma haikuwa rahisi kwa kuwa mtandao wa walioshiriki ujangili walikuwa na nguvu ya kufanya chochote wakati wowote, ikiwamo kutoa rushwa nyingi katika vyombo vya usimamizi wa sheria kama Mahakama na Polisi.

Kwa kipindi hicho baadhi ya vigogo wa serikali na taasisi zake walidaiwa kushirikiana na mtandao wa majangili duniani, kuwezesha kuuawa kwa wanyama na kisha kuchukua nyara na kuzisafirisha kwenye masoko ya nchi za Asia ambazo ni China, Vietnam na Thailand.

Watumishi wanaosimamia rasilimai hizo walijikuta kwenye wakati mgumu kwa kuwa ushahidi uliharibiwa wakati wa upelelezi kutokana na nguvu ya fedha, na walipofikishwa mahakamani waliachiwa, huku kukiwa na mashinikizo kutoka kwa wakubwa juu ya watuhumiwa waliokamatwa kuachiwa.

Kutokana na hali hiyo ujangili wa tembo na faru ulishika kasi na kutishia uwepo wa wanyama hao, huku baadhi ya maeneo yaliyohifadhiwa yakibaki na tembo wadogo, huku kukiwa na namna nyingi za kusafirisha nyara hizo kupita mipaka ya nchi.

Utashi wa kisiasa ni utayari wa viongozi wa kisiasa kupambana na jangili, jambo ambalo limewezekana sasa kwa kuwa kesi zinapelelezwa vizuri, watumumiwa wanakamatwa na kuhukumiwa, kila mmoja anawajibika katika eneo lake kwa kuwa utayari wa wanasiasa ni mkubwa na hakuna anayethubutu kuwepo kwenye mtandao wa ujangili.

Ni juhudi kubwa zinazopaswa kupongezwa sana kwa kuwa sasa wanyama watakuwa salama dhidi ya ujangili, na maana yake wataongezeka kama ambavyo faru wameongezeka na hali ikiwa hivyo upo uwezekano mkubwa wa kuirudisha Tanzania katika nchi zenye idadi kubwa ya wanyamapori hao.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja kuna ongezeko la faru 29, ambazo ni habari njema, huku kukiwa na mkakati wa kuongeza wanyama hao hadi 205 ifikapo mwaka 2023.

Faru ni mmoja ya wanyama walio hatarini kutoweka duniani, huku wengine ni mbwa mwitu wakitoweka kutokana na mgogoro baina ya binadamu na wanyama.

Ni hatua nzuri na muhimu sana kuhifadhi na kutunza wanyama hawa ili waendelee kuongezeka, hatua ambayo italeta watalii wengi ambao wataliingizia taifa mamilioni ya fedha.

Faru hao wanatunzwa kwa kutumia vifaa maalum walivyovalishwa vikionyesha mienendo yao na walipo,ikiwamo wakiugua taarifa hutolewa mapema, na kila siku taarifa zao zinachukuliwa lengo ni kuhakikisha usalama wa wanyama.

Wanyama hao walipungua kiasi cha serikali kununua wanyama hao kutoka Afrika Kusini, ambao waliwekwa katika Hifadhi ya Taifa Mkomanzi na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.


Kuendelea kutunza wanyama hawa kutapunguza gharama kwa serikali kununua na kuwatunza, na ongezeko hili ni mafanikio makubwa ambayo yatanufaisha taifa.

Ni muhimu utashi huu ukaenda moja kwa moja hadi kwenye ulinzi wa shoroba (mapito ya wanyama) na maeneo ya mtawanyiko ambayo imekuwa ngumu kutunza kutokana na kukosekana utashi wa kisiasa, kwa kuwa katika maeneo hayo kuna wananchi wanafanya shughuli za kibinadamu, lakini wasimamizi wa sheria wanashindwa kuzisimamia kutokana na kizuizi cha wanasiasa.

Ni muhimu kulinda maeno muhimu ya uhifadhi ili wanyama hawa waendelee kuongezeka kwa manufaa ya taifa, ni muhimu wakalindwa kwa nguvu zote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## Kuwapo madarasa ya kutosha inawezekana jamii zikiamua

Na Sabato Kasika

**KAMA** kawaida kila mwisho wa mwaka hekaheka za kuwaandikisha watoto kuanza darasa la kwanza zinapamba moto.

Wazazi na walezi sehemu mbalimbali wanakimbizana na wakati kuwasajili watoto ili kuanza shule Januari 2021.

Wakati wakiendelea na kazi hiyo, wanafunzi waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka huu, nao wako kwenye maandalizi ili Januari mwakani waanze kidato cha kwanza.

Hata hivyo, tatizo linalojitokeza kila mwaka ni uhaba wa madarasa kwa wanafunzi wapya hasa darasa la kwanza na kidato cha kwanza, na kusababisha serikali na wadau wa elimu kukuna vichwa.

Kuendelea kuwapo tatizo hilo kila mwaka, kunawaibua wadau wa elimu kushiriki kikamilifu kuwapatia wanafunzi madarasa ili kuondokana na tatizo hilo ili wahudhurie shuleni kikamilifu.

Ikumbukwe kuwa, wakati shule zikiwa mbioni kufunguliwa mwezi ujao, baadhi ya viongozi wa serikali wakiwamo wakuu wa wilaya za Handeni Tanga na Musoma wanaendelea jitihada za kukabiliana na tatizo. Jitihada hizo ni kuzunguka kwenye maeneo mbalimbali kuhamasisha uandikishwaji wa wanafunzi wa awali na darasa la kwanza, lakini pia kuhimiza ujenzi wa madarasa.

Si hao tu karibu nchi nzima kuna jitihada mbalimbali zinafanyika, ili wanafunzi wapya ambao wataanza shule Januari waondokane na usumbufu usio wa lazima.

Katika kufanikisha ujenzi huo wa madarasa, wazazi na walezi wanatakiwa kushirikishwa ili watambue kuwa shule za umma ni zao, hivyo wana wajibu wa kuzihudumia kadri inavyowezekana.

Iwapo kila mzazi na mlezi atashiriki kuboresha elimu katika eneo lake, wanafunzi wote hasa wa sekondari, wataanza masomo pamoja, badala ya awamu, hali ambayo inasababisha wengine kuwa nyuma kitaaluma.

Mtindo wa kuanza masomo kwa awamu usiwe ni mazoea, pengine tu wanapolazimika lakini inapowezekana, kila mmoja ashiriki kuboresha elimu kwenye eneo lake akitambua shule za umma ni mali ya wananchi.

Hivyo suala la wazazi na walezi kushiriki katika jambo hilo ni la muhimu ili kusaidiana na serikali kuboresha elimu, kwa kuchangia nguvukazi au vifaa ama fedha ili kusaidia watoto wao kuanza masomo kwa pamoja.

Ikitokea wakawapo baadhi ya wazazi na walezi ambao wanafanya kampeni usiku ya kukwamisha maendeleo ya ujenzi wa madarasa, wasipewe nafasi, badala yake waripotiwe kwenye mamlaka husika. Wakati mwingine inawezekana wakawapo watu aina hiyo, ambao wanasomesha watoto wao katika shule za kulipia, hao wasipewe nafasi ya kukwamisha maendeleo ya shule za umma.

Umefika wakati wa kuachana na mtindo wa wanafunzi kusoma kwa awamu, kutokana na uhaba wa madarasa, wakati wazazi na walezi wakiwa na uwezo wa kuchangia ujenzi wa madarasa lakini hawajengi.

Binafsi ninaamini kwamba, iwapo kila mmoja atatambua na kutimiza wajibu wake, uhaba wa madarasa na madawati hautaendelea kujirudia kila mwaka, badala yake utakuwa ni historia.

Ujenzi wa madarasa uwe ni endelevu kuanzia Januari hadi Desemba, ili wanapoandikishwa wanafunzi wapya au wanaoanza kidato cha kwanza, viongozi wahangaike huku na kule kuharakisha ujenzi huo.

Lakini, pia ni vyema serikali ikawa inatumia takwimu zake kutambua idadi ya wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza na wa kidato cha kwanza ili iwe rahisi kutambua uhaba wa madarasa na kuufanyia kazi.

Uhaba wa madarasa kila mwaka ni wazi unahitaji ufumbuzi kwa kujipanga vizuri zaidi ili kuepuka kuwaumiza wanafunzi na hasa wa kidato cha kwanza ambao huwa wanalazimika kusoma kwa awamu. Njia mojawapo ya kujipanga ni kushirikisha wadau wote wa elimu, hasa wazazi, huku serikali nayo ikitumia takwimu zao kutambua ukubwa wa tatizo na jinsi ya kulipatua ufumbuzi wa kudumu.

Kukiwa na mipango ya muda mrefu inayohusu kuangalia takwimu na matokeo ya mtihani wa taifa wa darasa la saba, itakuwa ni rahisi kujua idadi ya wanafunzi wanaotarajia kuanza kidato cha kwanza mwaka unaofuata.

Hayo yote yakisimamiwa inavyotakiwa, inakuwa ni rahisi wanafunzi wote kuanza shule bila ufumbufu, kwa kuwa limebaki jukumu la wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao shuleni ili waendelee na masomo

## HABARI KITAIFA

# Mwanafunzi wa kike aliyeibuka kidedea ufaulu ARU afunguka

**Na Elizabeth Zaya**



MWANAFUNZI wa kike, Jasmine Mndeme(23), aliyeibuka mwanafunzi bora zaidi kati ya wehitimu 926 wa Chuo Kikuu cha Ardhi(ARU) mwaka huu, amefunguka siri ya kufikia katika hatua hiyo.

Jasmine (pichani) amehitimu Shahada ya kwanza ya Usanifu Majengo, Jumamosi ya wiki iliyopita katika mahafali ya 14 ya chuo hicho jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Jasmine alisema miongoni mwa vitu ambavyo vimemsaidia kushika nafasi hiyo ni pamoja na kusoma kwa bidii, uvumilivu na kujituma, ubunifu katika masomo kwa vitendo, jitihada ya kutafuta msaada alipokutana na asiyoyajua pamoja na uchaguzi wa marafiki wanaopenda kusoma.

Alisema mwanzoni wakati anajiunga na kusoma kozi hiyo katika chuo hicho, alikutana na mambo magumu ambayo endapo angekuwa wa kukata tamaa asingefika hapo alipo.

"Mwanzoni kabisa wakati najiunga kusoma kozi hii, mambo yalikuwa magumu sana, kila kitu nilichokuwa nakutana nacho nilikuwa nakiona ni kigumu. Ilibidi nitulie na kutafakari kwanza ili niweke mikakati ni namna gani ninaweza kutoka hapo nilipo, nilikuwa najisemesha na kukataa mwenyewe kurudi nyuma na kuonekana nimeshindwa kabisa," alisema Jasmine.

"Niliwaza kwamba chuoni pale kulikuwa na watu wengine wanaosoma kozi kama yangu ambao walikuwa wamenitangulia, niliamua kwamba nitafute marafiki wazuri ambao si tu wataishia kuwa marafiki bali watakuwa ni wenye uwezo mkubwa katika kozi ninayosoma na ambao watakuwa tayari na mimi wakati wote ninapohitaji msada wao katika masomo yangu."

"Na hapo ndipo nilianza kuamua kuwa lazima nifanikiwe katika hili, nilipambana, nikapata watu ambao walikuwa wazuri kwelikweli katika kozi ninayosoma mimi, nashukuru walinisaidia kwa kiwango kikubwa na nikaona kwamba katika safari yangu hiyo, hakuna kitakachonishinda. Walimu wetu wanaotufundisha ni wazuri sana, lakini niliona hawawezi kuwa na muda mwingi wa kusumbuliwa kama ilivyo kwa ma rafiki."

"Baada ya kuonyeshwa mwanga, nilianza kupambana, nilihakikisha najitoa kwa nguvu zote kutafuta material ya kila maswali niliyokuwa nayo. Kozi yangu inahitaji ujitoe kwelikweli, kwa hiyo wakati mwingine nilikuwa nakosa hata muda wa kulala usingizi na kula."

Alisema alama alizokuwa akipata katika masomo yake ilikuwa si chini ya B+.

Jasmine alisema aliipenda zaidi kozi yake kwa sababu ilikuwa inahuisisha vitendo zaidi kuliko nadhalia.

"Kozi yangu inahusisha vitendo zaidi, kwa hiyo ilinisaidia kunijenga kwa sababu nilikuwa napenda kazi yangu yoyote inayopita mikononi mwangu niifanye kwa ufanisi wa hali ya juu, nilikuwa sijali zaidi kuhusu alama ninazopata kuliko ile kazi ya vitendo ninayofanya, kukesha ilikuwa kama sehemu ya maisha kwangu,"alisema Jasmine.

"Kozi yangu ilikuwa kama ndoa, yaani wakati wote unatakiwa lazima uwe nayo, iwe uko chuoni au popote na kama unavyojua majengo kila mahali yanatuzunguka, kwa hiyo suala la kujifunza kwa kozi yangu niliifanya wakati wote."

"Nakumbuka wakati tangu nikiwa mdogo nilikuwa napenda kubuni vitu na nilikuwa kila kitu ninachokiona mbele yangu natamani kukichora hata kama siyo kwa uzuri wake, kwa hiyo niliweka jitihada kubwa sana kwa sababu pia ilikuwa ni 'passion' yangu. Nashukuru Mungu kwa hili nilijikuta nimeipenda zaidi kuliko hata nilivyoanza mwanzo wakati ndio naingia chuo."

Jasmine anawashauri wanafunzi wengine wa kike, kuhakikisha kwamba wanaweka juhudi, maarifa na ubunifu katika kila jambo wanalopenda kulifanya.

Anawashauri pia wazazi, kuwaruhusu watoto wao kusoma kozi wazoziopenda.

"Kwetu sisi tuko watoto watatu, nakumbuka wazazi wangu walikuwa wanataka nisome kozi ya uhandisi, lakini nilipowaambia kwamba nasoma usanifu majengo hawakuelewa japokuwa baadae walikuja kunielewa na kuniunga mkono. Wasichana wengi wanaogopa kusoma kozi kama hizi wakihofia ni ngumu, hakuna kitu kigumu pale unapoweka juhudi na bidii,"alisema Jasmine.

# Ofisa tabibu jela miaka 3 kwa kuomba rushwa ya 30,000/-

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imemhukumu Ofisa Tabibu wa Kituo cha Afya Katoro, Lameck Kuzenza (25), mkazi wa Katoro kutumikia kifungo cha miaka 3 jela kwa makosa mawili ya kuomba na kupokea rushwa ya Sh 30,000.

Alipokea fedha hizo kutoka kwa Saidi Kulwa ili kumufanyia usafi wa mimba iliyukuwa imearibika ya mke wake, Sheha Hashimu, kinyume na kifungu cha 15(1)(a) na (2) cha sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329 ya mwaka 2019.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Obadia Bwegoge, baada ya ushahidi uliyotolewa na upande wa mashtaka kuthibitisha makosa hayo pasipokuacha shaka yoyote.

Hakimu Bwegoge alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwa waunguzi wengine wenye tabia ya kikatili kama yake.

Awali, upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoa wa Geita, Augustino Mtaki, alidai hapo mahakamani kuwa walipeleka mashahidi 6 na vielelezo 4 ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo.

Hakimu huyo alisema mama huyo alifika hospitalini hapo Desemba 12, mwaka 2019 majira ya asubuhi kwa ajili ya kuchunguzwa maumivu ya tumbo ambayo yalikuwa yakimsumbua na alikuwa afanyiwe kipimo cha 'Utra sound' hospitali ya Izengo Katoro.

Aidha, alisema baada ya ushauri huo alirudi hospitalini hapo akiwa na majibu vipimo yaliyoonyesha kwamba ujauzito wake ulikuwa umearibika, hivyo alitakiwa kusafishwa na mshtakiwa huyo, ambaye alimwambia mume wa mama huyo.

Alisema mume wa mama huyo hakuwa na fedha za matibabu, hivyo alienda kutafuta hizo fedha, lakini hakuzipata, na kwamba badaye alikuja kubaini kuwa huduma ya kusafisha ujauzito uliyoaribika ni bure.


AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
benki kwa maendeleo yako

## NOTISI / TANGAZO

CHAMPION AUCTION MART LTD, SUNDI AUCTION MART LTD, SMARKCORE GROUP LTD, NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO. LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, MASETO AUCTIONEERS AND DEBT COLLECTORS LTD, BEST GROUP LTD SALEI AUCTION MART LTD kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| S/N | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | JOHN JOSEPH NYAMGINI | JOHN JOSEPH NYAMGINI | NYUMBA | NYAMUHONGOLO-MWANZA | 05/01/2021 NAKUENDELEA |
| 2 | WANJERU CONSTRUCTION CO. LTD | IDD MOHAMED | TITTLE NO. 23519, L.O NO. 1338 BLOCK 'M' | PASIANSI-MWANZA | 28/12/2020 NAKUENDELEA |
| 3 | LWEYEMAM MEDARD KABENDERA | LWEYEMAM MEDARD KABENDERA | TITTLE NO. 74288, L.O NO 542135, PLOT NO. 318, BLOCK 'A' | NYASHISHI | 28/12/2020 NAKUENDELEA |
| 4 | RENATUS CHRISTIAN PETRO | RENATUS CHRISTIAN PETRO | KIWANJA | MIGANGA KATA YA MKONTHE-DODOMA | 28/12/2020 NAKUENDELEA |
| 5. | VICTOR MOSSES NNKO | ARISTIDEUS RICHARD MALYA | NYUMBA | KIBAIGWA MTAA WA MAJENGO-DODOMA | 28/12/2020 NAKUENDELEA |
| 6. | RUTTA GODFREY RWECHUNGURA | RASHID ATHUMANI MWENDI | NYUMBA | MUIMWA-DODOMA | 29/12/2020 NAKUENDELEA |
| 7. | TITO KALAM SANGA | TITO KALAM SANGA | NYUMBA | KITONGOJI CHA KARUME-KIBAIGWA-DODOMA | 30/12/2020 NAKUENDELEA |
| 8 | JULIUS KALANGA LAIZER | JULIUS KALANGA LAIZER | PLOT NO. 802 & 803, BLOCK 'N' | MJI MPYA STREET – MONDULI -ARUSHA | 28/12/2020 NAKUENDELEA |
| 9 | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NAMBA YA HATI -46357 MBYLR, L.O NO. 505295, L.D NO. –TDM/4481PLOT NO. 54 & 55, KITALU NA. C | TUNDUMA | 28/12/2020 NAKUENDELEA |
| | | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NAMBA YA HATI; 47332-MBYLR, L.O.NO.788027, KIWANJA NO. 160, KITALU NA;N | TUNDUMA | 28/12/2020 NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papohapo baada ya mnada kumalizika. Na 75% itakayoba kitalazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigiesimu no. 0754 497 396 / 0752 000 695
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilicho wekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.



Wafugaji wa Kijiji cha Lusilile, Wilaya ya Manyoni mkoani Singida wakimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya hiyo Charles Fussi (hayupo pichani) mwishoni mwa wiki. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mkumbo aitaka TIC kuthamini wawekezaji

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amewataka watumishi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kumthamini mwekezaji anayetaka huduma yao na achukuliwe kuwa mtu muhimu, mlipa kodi anayekuja kuzalisha ajira na kukuza pato la taifa.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo jana baada ya kutembelea ofisi za TIC na kuzungumza na watendaji wake huku akiwakumbusha dira ya miaka mitano lengo lake ni kuhakikisha uchumi katika sekta rasmi na isiyo rasmi unakuwa kwa asilimia nane kwa mwaka na kutoa ajira milioni nane kwa kipindi cha miaka mitano.

Alikitaka kituo hicho pamoja na mambo mengine kihakikishe kinaongeza jitihada za kutambulika zaidi duniani.

Alisema hatua ya kwanza ni lazima serikali na sekta binafsi zifanye kazi kwa pamoja kwa kusikilizana, kuheshimiana, kuaminiana na kushirikiana kwa sababu wanategemeana.

Prof. Mkumbo alisisitiza wasimchukulie mwekezaji kama mtu mwenye shida badala yake apewe utaratibu wa wazi unaoeleweka na vigezo vinavyotakiwa kwenye uwekezaji.

Aliitaka TIC iimarishe uratibu na uhusiano na taasisi nyingine ambazo zinahusika na uwekezaji.

"TIC ni uratibu hivyo lazima tujenge uwezo wa ushawishi siyo wa shurutishi ni wa kushawishi wenzetu tunaofanya nao kazi tubadilishe mitazamo yao, badala ya kuwawezesha wawekezaji wanawadhibiti, kazi yao siyo kumkwamisha mwekezaji bali kumsaidia," alisema.

Kadhalika, Prof. Mkumbo alisema mwelekeo wa nchi kwa miaka mitano ijayo ulitolewa Novemba 13, wakati Rais John Magufuli akizindua Bunge 12 mjini Dodoma.

"Katika hotuba yake yenye kurasa 41, ukurasa wa tisa mpaka 31 ulizungumzia uchumi na alitoa malengo mengi ya kiuchumi, lakini makubwa mawili ambayo tunaweza kuyaita 8/8, nane ya kwanza ni uchumi wa nchi unakua angalau kwa asilimia nane kwa mwaka katika miaka mitano, nane ya pili, Rais Magufuli anataka kuona uchumi katika sekta rasmi na isiyo rasmi unazalisha ajira zisizopungua milioni nane," alisema.

Prof. Mkumbo alisema Rais alielekeza njia kuu ya kufikia malengo hayo ni kuvutia wawekezaji wa ndani na nje.

"Kwa dunia ya sasa ushindani wa kukuza uchumi upo katika eneo la kuvutia wawekezaji ambapo mataifa mawili duniani China na Marekani yamefanikiwa katika hilo, kwa Afrika mataifa yanayoongoza kiuchumi ni yale yanayovutia wawekezaji."

"Hili eneo la uwekezaji ni la msingi ndiyo maana Rais analisisitiza, kuvutia wawekezaji kuna mazingira ya asili ambayo Tanzania tumejaaliwa tumezungukwa na nchi nane hazina bandari, lakini hatupo peke yetu wenye bandari."

Kazi kubwa ya kufanya Prof. Mkumbo alisema wawekezaji wanaangalia idadi na ubora wa wafanyakazi na angalau serikali wana uhakika zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania wamepata elimu ya msingi ambayo sasa inakwenda hadi kidato cha nne.

"Eneo la kuboresha ni ufundi na teknolojia ili watu wetu wawe na ujuzi unaokubalika, ila kwa maana ya kiwango cha malipo tunavutia kwa sababu gharama za mfanyakazi hapa kwetu ni nzuri ikilinganishwa na maeneo mengine," alisema.

Alisema eneo la msingi ambalo linatakiwa kufanyiwa kazi ni la mtazamo wa watumishi wa umma, serikali kwa ujumla na upande wa wawekezaji.

# Biteko afuta leseni saba, asimamisha kazi watatu

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SAKATA la utoroshaji wa madini wilayani Chunya, mkoani Mbeya, limechukua sura mpya baada ya Waziri wa Madini, Dotto Biteko, kuwasimamisha kazi watumishi watatu wa Tume ya Madini kituo cha Chunya, kumvua madaraka Mwenyekiti wa Soko la Madini la Mkoa wa Kimadini Chunya na kufuta leseni za wanunuzi saba wa dhahabu.

Waziri Biteko alifanya uamuzi huo jana alipokuwa akizungumza na wachimbaji wadogo wa madini katika kikao kilichofanyika jijini hapa ikiwa ni siku chache baada ya maaskari wawili na raia mmoja kupandishwa kizimbani kwa tuhuma za kutorosha madini.

Alisema kuanzia mwezi wa Agosti mwaka huu, Wilaya ya Chunya imekuwa kinara wa utoroshaji wa madini nje ya nchi hali iliyosababisha serikali kufanya uchunguzi na kubaini watumishi hao kuhusika kwenye vitendo hivyo.



Biteko (pichani) alihusisha tuhuma hizo za utoroshaji wa madini na tukio la hivi karibuni la askari wawili wa Jeshi la Polisi na mfanyabiashara mmoja wa madini waliofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, wakituhumiwa kushirikiana kutorosha madini ya dhahabu yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.8.

Alisema baada ya serikali kufanya uchunguzi wa kina imewabaini wafanyabiashara hao saba kuhusika na matukio ya utoroshaji madini na ndio sababu imeamua kufuta leseni zao.

"Kwa mamlaka niliyonayo nimeamua kumvua madaraka mwenyekiti wa soko la madini la hapa Chunya na pia wafanyakazi watatu wa Tume ya Madini waliokuwa hapa Chunya, nimewasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi, lakini pia leseni za wafanyabiashara ambao tumebaini wanahusika na utoroshaji wa madini nimezifuta kuanzia sasa," alisema Biteko.

Vile vile, Waziri Biteko aliagiza mawakala 13 wa wanunuzi wa dhahabu katika maeneo mbalimbali wilayani hapo kwenda polisi kujisalimisha ili wahojiwe kuhusu tuhuma za utoroshaji wa madini.

Biteko pia aliagiza maeneo yote ya kuchenjua dhahabu kwa kutumia mercury (zebaki) maarufu kama mialo, yasajiliwe ili iwe rahisi kudhibiti dhahabu inayopatikana huko.

Baada ya agizo hilo la waziri, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alianza utekelezaji mara moja kwa kumtaka Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ulrich Matei, kuwakamata wote waliotajwa na waziri.

"Naagiza RPC uanze utekelezaji mara moja, hawa watumishi watatu pamoja na mwenyekiti wa soko la madini wakatwe na kuwekwa ndani ili wakahojiwe na pia hata wale 13 ambao waziri ameagiza wakajisalimishe wenyewe polisi wasihangaike kwenda, wala wasitumie mafuta yao kwenye magari kwenda polisi, mimi naagiza wakawakamate huko huko walipo," alisema Chalamila.

Pia, aliwataka maofisa wa madini kuanza usajili wa mialo ya kuchenjua dhahabu kwa kutumia mercury na kutaka zoezi hilo likamilike mara moja.

Chalamila alisema, tukio la utoroshaji wa madini limeuchafua Mkoa wa Mbeya, kwamba hata yeye anatamani aende mwenyewe polisi akawekwe mahabusu.

Awali, Mwenyekiti wa Chama Cha Wachimbaji wa Madini, Wilaya ya Chunya, Leonard Manyesha, alisema kuwa dhahabu nyingi inayochenjuliwa kwenye mialo ndiyo inayotoroshwa kwa vile haina udhibiti wowote hasa katika upatikanaji wa kumbukumbu zake.

Manyesha aliishukuru serikali kwa kuchukua hatua kali dhidi ya watu wanaojihusisha na utoroshaji wa dhahabu na kuwa hali hiyo inaikosesha serikali mapato ingawa imejitahidi kufuta kodi nyingi kwenye sekta ya madini na kuwawekea mazingira mazuri ya kuchimba na kufanya biashara ya dhahabu.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Matei, alisema msako umeanza na zaidi ya watu 40 wametiwa mbaroni.

# Kero ya maji kuwa historia Tarime mwakani

**Na Timothy Itembe,** TARIME

WANANCHI Wilaya ya Tarime mkoani Mara, wametakiwa kutunza miradi ya maji inayoendelea kutekeleza kwenye maeneo yao pamoja na miundombinu yake ili idumu na kupunguza changamoto zilizopo.

Akizungumza na waandishi wa habari, mjini Tarime, Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Sebastian Marwa, alisema kuna baadhi ya watu wanahujumu miradi inayotekelezwa badala ya kuitunza ili kupunguza changamoto iliyopo.

Meneja huyo aliongeza kuwa wananchi watarajie kuondokana na kero ya maji ifikapo 2021, baada ya miradi ya maji inayotekelezwa kutekelezeka kupitia fedha za serikali ifikapo Juni mwaka 2021.

Meneja huyo alibainisha miradi inayotegemewa kukamilika ili wananchi kuondokana na kero ya upatikanaji wa majisafi na salama ni ujenzi wa mradi wa maji wa Sirari katika vijiji 4 vikiwamo Buriba, Sokoni, Mpakani na Kanisani.

Mradi mwingine ni ukarabati wa mradi wa maji Magoto katika vijiji vya Magoto na Nyakonga ukiwamo ujenzi wa mradi wa maji Nyakonga pamoja na uchimbaji wa visima sita Halmashauri ya Mji wa Tarime.

"Jumla ya Sh. bilioni mbili zitatumika katika kutekeleza miradi ambayo, huku lengo likiwa ni kupata vyanzo vya kujenga miradi, mitandao midogo midogo ya upatikanaji wa maji," alisema Mtaza.

Mtaza alisema kuna miradi mingine inayotarajiwa kuanza ambayo ni ukarabati wa mradi wa maji Keisangura, Nyamwaga, Gibaso, Kewanja na Borega (A).

Aidha, alisema ujenzi wa mradi wa maji wa Nyantira na Nyansicha inatarajiwa kuanza ifikapo Januari, 2021.

Alibainisha kuwa kuna miradi ambayo imekamilika na wananchi wanaendelea kunufaika na huduma hiyo ambayo gharama yake inafikia Sh. milioni 479 katika vijiji vya Nyarero, Korotambe, Gamasara na ukarabati wa pampu za mkono 65 zinazohudumia vijiji 42.

# Kanisa lamwomba JPM kusimamia uchumi

**Na Julieth Mkireri**

KANISA la Pentecostal Motomoto lililopo Boko Jimbo, limemuomba Rais John Magufuli kusimamia ukuaji wa uchumi kwa kila sekta ili kuondoa umasikini wa kipato.

Hayo yameelezwa juzi kanisani hapo wakati wa ibada maalumu ya kumshukuru Mungu na kumpongeza Rais Magufuli kwa kuchaguliwa kuongoza nchi kwa mara nyingine na baraza lake la mawaziri alilolitangaza hivi karibuni.

Askofu wa Kanisa hilo, Eliasaph Mattayo, alisema Kanisa hilo linamwomba Rais kuendelea kusimamia ukuaji wa uchumi katika kila sekta, kuondoa umasikini wa kipato na kuhakikisha uvunaji wa rasilimali vinawanufaisha Watanzania wote, Serikali yake inaweza kufanya maajabu katika miaka mitano mingine.

**Wakati nasubiri muda wangu alionipangia Mungu siwezi kulala, naendelea na maombi kumshukuru Mungu na kufanya kazi, kwani Mungu ametupa bahati kuabudu katika nchi yenye amani.**

Alisema Kanisa hilo pia linawapongeza wagombea waliokubali matokeo ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

" Ibada hii inagusa vitu muhimu katika nchi yetu, tunashukuru Mungu kwa muda huu amepatikana mmoja ambaye amemchagua... kilichobaki ni kutii mamlaka zilizopo kwani usipotii hizo huwezi kumtii kiongozi wa kanisani, tuendelee kumshukuru Mungu kwa amani iliyopo," alisisitiza.

Aidha, katika ibada hiyo ambayo ilihudhuriwa na aliyekuwa mmoja wa wagombea urais kupitia Chama cha ADC, Queen Sendiga, Askofu alimtaka kuendelea kusimamia katika maombi kwani kila jambo Mungu ndiye anayeamua.

Akishukuru kwa mualiko wa kushiriki ibada hiyo ya kuiombea nchi na kumpongeza Rais, Queen alisema uongozi unatoka kwa Mungu na kwa muda aliopanga, hivyo hanabudi kushukuru na kuendelea na majukumu mengine, huku akiwahakikishia waumini wa dini zote kuendelea kushirikiana nao pale watakapomuhitaji.

"Wakati nasubiri muda wangu alionipangia Mungu siwezi kulala, naendelea na maombi kumshukuru Mungu na kufanya kazi, kwani Mungu ametupa bahati kuabudu katika nchi yenye amani," alisema.

Kanisa hilo pia liliwaombea viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Mwinyi.



Waziri wa Viwanda na Biashara ambaye pia ni mbunge wa Masasi mjini, Geofrey Mwambe( kulia) akiteta jambo na katibu Tawala Mkoa wa Mtwara, Alfayo Kidata, walipokutana katika kikao cha baraza la madiwani la Halmashauri ya mji Masasi jana, kilichofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Uuguzi na Ukunga Masasi. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Mbunge kukopesha wananchi bila riba

**Na Shaban Njia,** NGARA

MBUNGE wa Ngara mkoani Kagera, Ndaisaba Ruhoro, ametenga Sh. milioni 50 kwa ajili ya kuwakopesha wananchi mikopo isiyokuwa na riba ili kukuza mitaji yao na kuondokana na utegemezi kwenye familia zao.

Pia alisema kiasi hicho kitasaidia kupunguza msongamano wa mikopo isiyokuwa na riba kutoka Halmashauri ya Ngara, ambayo imekuwa ikitoa mikopo asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa vijana, kinamama na watu wenye ulemavu.

Ndaisaba aliyabainisha hayo wakati akizungumza na wananchi wa kata tatu za Kinazi, Mugoma na Kirushya akiwa ameambatana na kamati ya ushauri na maendeleo ya jimbo akisikiliza kero za wananchi hasa katika sekta ya afya, elimu, barabara na kilimo.

Alisema ameanzisha mfuko wa kuwakopesha wananchi mikopo isiyokuwa na riba na kiasi cha Sh. milioni 50 zimeshatengwa, hivyo wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo watapata mikopo nafuu isiyo na riba kwa ajili ya kujiendeleza na kukuza mitaji yao.

"Nitateua kamati maalum ya wazee itakayokuwa na jukumu la kupitia na kuthibitisha majina ya watu wanaohitaji kupewa mikopo isiyokuwa na riba, niwaombe mfuko utakapofunguliwa vijana, kinamama na watu wenye ulemavu wajitokeze kwa wingi kuchangamkia fursa hii," alisema.

Aliongeza:" Nitatoa msaada wa mabati kwa ajili ya kuezeka ghala la mazao ili wananchi wapate sehemu ya kuhifadhi mazao yao wanayoyapata wakati wa mavuno hasa zao la kahawa...mikopo mtakayopata hakikisheni mnazielekeza kwenye shughuli mlizopanga na sio kwenye anasa."

Felix Peter, Mkazi wa Mugoma, alisema kitendo cha mbunge kuanzisha mfuko wa kuwakopesha wananchi mikopo isiyokuwa na riba kinafaa kuigwa na wabunge wengine na kwamba utasaidia kupunguza malalamiko ya wananchi wanaokosa mikopo Halmashauri kwa kukosa vigezo.

# Wachangamkia mbegu bure za kisasa michikichi

**Na Ashton Balaigwa,** KIGOMA

WAKULIMA katika halmashauri mbalimbali mkoani Kigoma wamejitokeza katika kituo cha Utafiti wa Kilimo (TARI) Kihinga mkoani Kigoma, kuchukua mbegu bora za kisasa za michikichi zinazotolewa bure na Serikali.

Kituo hicho cha mpaka sasa kimeshazalisha miche milioni 4.2 aina mpya ya tenera kwa gharama ya Serikali na kuigawa bure kwa wakulima wa Mkoa wa Kigoma.

Akizungumza wakati wa ugawaji wa mbegu hizo, Kaimu Mkurugenzi wa TARI Kihinga, Filson Kagimbo,alisema pamoja na kugawa mbegu hizo bure kwa wakulima, wameshagawa katika Halmashauri sita kati ya nane zilizopo mkoani Kigoma ikiwemo, Halmashauri za Kasulu, Kigoma, Kasulu Mji, Uvinza, Kigoma Manispaa na Buhigwe.

**Kituo hicho cha mpaka sasa kimeshazalisha miche milioni 4.2 aina mpya ya tenera kwa gharama ya Serikali na kuigawa bure kwa wakulima wa Mkoa wa Kigoma.**

Dk. Kagimbo alisema pamoja na kusambaza mbegu hizo katika Halmashauri hizo, kituo cha TARI Kihinga kimeendelea kuzalisha miche hiyo kwa ajili ya kugawa bure na kuwafundisha wakulima kilimo hicho cha michikichi.

" Sisi kama watalaam pamoja na kuzalisha miche ya michikichi, tumeamua kuweka kitalu cha miche hapa kwenye jengo letu ili kuwafundisha wakulima wanaotutembelea tunawapa bure baada ya kupata utalaamu wa kilimo cha michikichi.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, DK. Geofrey Mkamilo, alisema,uzalishaji wa miche ya michikichi unaoendelea kufanywa na kituo hicho umesaidia kuokoa mabilioni ya fedha za Serikali kwa kuwa mche mmoja wa tenera unagharimu kiasi cha Sh.10,000 kila mmoja.

Dk. Mkamilo,alisema ugawaji wa mbegu hizo bure umelenga kuongeza uzalishaji wa mafuta yanayotokana na michikichi ili kuisaidia kuokoa fedha za serikali zinazotumika kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi na badala yake yazalishwe hapa nchini.

Alisema serikali imekuwa ikitumia zaidi ya Sh. bilioni 400 kwa mwaka kwa ajili ya kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi, hivyo mkakati ulipo wa serikali ni kuhimiza uzalishaji wa michikichi katika Mkoa wa Kigoma na mikoa mingine ya jirani kusaidia kuokoa fedha kwa kuzalisha michikichi kwa wingi .



Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga wakila kiapo cha kuwa madiwani kamili, mara baada ya kushinda kwenye uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, kiapo hicho kimefanywa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Kishapu, Amana Ismail. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 40 waibuka kidedea droo kampeni NMB

**Na Beatrice Moses**

WASHIRIKI 40 wametangazwa washindi 40 wa Sh. 100,000 kila mmoja wa droo ya pili ya Kampeni ya NMB MastaBata 2020, inayochagiza matumizi ya Kadi za NMB Mastercard na Masterpass QR miongoni mwa wateja wa benki hiyo.

NMB MastaBaata, ni kampeni ya miezi mitatu iliyozinduliwa Novemba 24, mwaka huu, ambako zawadi mbalimbali zinatolewa zikiwamo za fedha, simu janja 'smartphone', jokofu, runinga pamoja na safari ya kwenda kupumzika Zanzibar, Serengeti na Ngorongoro.

Droo ya pili ya kampeni, ilifanyika Makao Makuu ya NMB, jijini Dar es Salaam, chini ya usimamizi wa Mkaguzi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Rasuli Masudi, aliyewahakikishia washiriki na washindi mchakato unaozingatia sheria zote kuwapata.

Meneja Mwandamizi wa Idara ya Biashara za Kadi wa NMB, Manfredy Kayala, alisema katika kipindi chote cha kampeni hiyo, watakabidhi zawadi kwa jumla ya washindi 40 watakaojishindia fedha taslimu 100,000 kila wiki.

Pia, alifafanua kuwa NMB MastaBata itawazawadia washindi 15 simu janja aina ya Samsung Galaxy Note20, yenye thamani ya Sh. 2,480,000 kila mwezi, pamoja na zawadi kuu itakayotolewa katika fainali ya kuhitimisha kampeni hiyo.

"Zawadi kubwa kwenye kampeni hii ni ile ya washindi 15 pamoja na wenza wao kushinda safari ya utalii wa ndani iliyolipiwa kila kitu na NMB, ambapo mshindi na mwenza wake watapata nafasi ya kutembelea Zanzibar, Serengeti na Ngorongoro," alisema.

"Aidha, washindi wa fainali tutawapa ruksa ya kuchagua utalii wa ndani au kuchukua zawadi mbadala kama runinga iliyolipiwa DSTV miezi mitatu, Jokofu la Milango Miwili, kompyuta Mmakato, simu janja (Samsung A70), water dispenser na microwave," alisema Kayala

Katika droo hiyo ya Ijumaa Desemba 11, washindi 40 waliotangazwa na kupigiwa simu ni Samwel Kilua, Mgonja Tumaini, Msindai Wazael, Saria Fulgence, Joachim Mabula na Alex Katanda.

# Mil. 165/- kukusanywa kutoa huduma za afya

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

ZAIDI ya Sh. milioni 165 zinatarajia kukusanywa ili kusaidia kutoa huduma za afya.

Huduma hizo ni za kupunguza vifo vya mama na mtoto, uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya vinywa kwa watoto waishio katika mazingira magumu na kusaidia upasuaji kwa jamii isiyokuwa na uwezo.

Hayo yalibainishwa juzi Jijini Mwanza na Mwenyekiti wa Kamanga Healthcare Foundation ambaye pia ni Daktari bingwa wa watoto, Dl. Mercy Minde, wakati akitambulisha majukumu ya asasi hiyo na kutafuta mchango kwa wadau.

Alisema fedha hizo zitatumika katika miradi minne ikiwamo kupunguza vifo vya wajawazito hasa wakati wa kujifungua wakianza na Mkoa wa Mwanza.

Alisema wanatarajia kutumia njia mpya ya kiteknolojia kwa kufuatilia vipimo wakati za ukuaji wa mtoto tumboni na kabla ya kuzaliwa.

Alisema miradi hiyo inatarajia kuchukua mwaka mmoja kukamilika kwa malengo ambayo asasi imejiwekea wakiamini wanaweza kuwafikia watoto takribani 600.

Aliongeza kuwa malengo waliyojiwekea ni kufikia asilimia 75 ya watoto wenye changamoto na asilimia 25 wenye uhitaji wa matibabu husika.

# Madiwani wanolewa sheria na kanuni

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

MADIWANI wa Halmadhauri ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wametakiwa kuzisoma sheria na kuzifafanua kanuni ili kufanya kazi zao kwa weledi.

Hayo yalisemwa na Gerard Zephyrin katika semina ya siku mbili, ambayo uliandaliwa kwa madiwani hao.

Gerard ambaye alikuwa mkufunzi katika semina hiyo ya siku mbili, aliwataka madiwani kujikita katika kuzisoma sheria na kuzifafanua vizuri kanuni mbili walizopewa ambazo ni maadiki na za kudumu za halmashauri ili waweze kufanya kazi kwa weledi.

"Kuzijua vizuri kanuni itawasaidia hata kuzijua haki zenu, ikiwamo na kuwasaidia kujua kuliendesha baraza lenu kwa kufuata kanuni hizo," alisema.

Mwenyekiti wa Halmadhauri ya Mkuranga, Mohamed Mwela, aliwataka madiwani kuyazingatia yote waliyofundishwa na kuwataka kwenda kuyafanyia kazi ili kuleta mafanikio kwa wananchi wa kata zao.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Filbeto Sanga, aliwata madiwani kuachana na makundi na kuwa na umoja ili kuwaletea wananchi maendeleo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 15, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

**TAKUKURU yakunjua makucha wala rushwa ngono miaka 20 jela**



Ukurasa 13

'Tamu, chungu' za sheria vikwazo ulinzi mazingira



Ukurasa 14

**RPC, hakimu ni majemedari wapya mapambano shuleni**

ELIMU

**NA MWANDISHI WETU**

## SIMULIZI....

# Ndivyo 'tochi' ilivyompa mwanafunzi ulemavu

"NILIKUWA na bidii na nilisoma kwa jitihada mchana na usiku. Baada ya kujifunza darasani na baadaye 'prep', nilijiongeza kusoma zaidi usiku nikutumia tochi."


"Kilichonisukuma ni kutamani kufanya vizuri na kuwa na mafanikio kielimu . Hata hivyo mwaka 2013 uliandika historia katika maisha yangu. Nilishindwa kusoma , si ubaoni au kitabuni. Sikuona herufi wala michoro kwenye vitabu nikalazimika kufungua ukurasa mpya"

Anasema mwanafunzi Joseph Machari, akisema kuwa hili lilimfanya atumbukie kwenye kundi la wenye uoni hafifu unaelekea kusababisha upofu, ukubwani.

Ni kutokana na hali hiyo akaanza rasmi kutibu macho. Alipatwa na masahibu hayo akiwa kwenye shule moja jijini Dar es Salaam, kabla ya kuhamia Sekondari ya Tusiime anakosoma sasa.

Anasema alikwenda kwa mabingwa kusaka matibabu lakini bila mafanikio kwani hakuweza kusoma tena na ilifika kipindi akalazimika kuacha shule.

"Niliacha shule na kuanza kujifunza masomo ya nukta nundu (breil) kwenye moja ya shule zenye wanafunzi wanaoishi na ulemavu wakiwamo wasioona na wenye uoni hafifu jijini Dar es Salaam. Nilifanikiwa kujua matumizi ya lugha hiyo na ndiyo ninayoitumia" anasema Joseph ambaye yuko kidato cha tano akisoma mchepuo wa sanaa masomo ya historia, jografia na fasihi (HGL).



Joseph Machari (kulia) pamoja na mwalimu wa taaluma John Kashefu, wakati wa utoaji wa tuzo kwa wanafunzi bora kitaifa. **PICHA: MWANDISHI WETU.**

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni shuleni Tusiime, anasema kusoma nukta nundu kuliigharimu familia yake zaidi ya Sh. 300,000 kwa miezi mitano.

Baada ya hapo aliimudu lugha hiyo na kueleza kuwa yeye ni miongoni mwa wanafunzi wengi na Watanzania wengi ambao wanapata uoni hafifu na hata upofu ghafla ukubwani, lakini hawawezi kupata mafunzo ya nukta nundu kwa sababu ya kushindwa kujilipia.

Anasema licha ya kwamba familia yake inamhudumia na kumsaidia anaamini kuna wengine wengi wanaohitaji msaada.

**KUPONZWA NA TOCHI**

Mwanafunzi huyu anasema wakati akitafuta tiba iligundulika kuwa katika kujibidisha kwenye kufikia elimu bora na kuwa mwanafunzi mwenye mafanikio kuna nyakati alitumia tochi kusoma usiku gizani.

Anasema mwanga ule kidogo unaozungukwa na giza kubwa unaweza kuwa sababu ya kutosha ya kuharibu lenzi na misuli ya macho.

Maelezo yake yanapatikana pia katika mtandao wa masuala ya afya unaonyesha kuwa kusoma maandiko kwa kutumia tochi usiku kuna athari kwa macho kwa vile hakuna tofauti na kusomea gizani.

Mtaandao unaeleza kuwa kuwa tochi inatoa mwanga kidogo unaojulikana kama 'spot light' inayomulika eneo dogo na hausambai sehemu kubwa hivyo kuwacha msomaji 'gizani' licha ya kwamba kuna mwanga.

Mtandao unasema kusoma huko kunadhoofisha misuli ya macho, kunaharibu kioo au lenzi na matokeo ya uoni hafifu na wakati mwingine kushindwa kuona kakamilifu lakini hakuna maelezo ya moja kwa moja kuthibitisha kuwa kusomea kwenye mwanga hasa wa tochi iwe ya betri au ya simu au kompyuta na pengine kusoma muda mrefu kunasababisha upofu.

Hata hivyo, mabingwa wa macho wanatahadharisha kuwa kusoma na mwanga wa tochi, au kusomea gizani kwa kutumia mshumaa, pengine mwanga wa kompyuta kunasababisha jicho kufanyakazi ya ziada kwa hiyo kunachangia kudhoofisha uwezo wa macho na kusababisha uoni hafifu hasa kwa watoto na wanafunzi shuleni.

**ALICHOJIFUNZA**

Joseph anasema akiwa kwenye changamoto hiyo, amegundua kuwa ni vigumu kupata elimu ikiwa una uoni hafifu. Unahitaji msaada mkubwa.

Anasema huwezi kuandika na kusoma unapokwama kama ilivyotokea kwake kwa vile unakuwa na uoni hafifu au matatizo ya macho ukubwani, kwa sababu mara nyingi unakuwa huna elimu wala ujuzi wa kutumia maandishi ya nukta nundu.

Anasema kuwa amejifunza kuwa hakuna vitabu wala machapisho ya nukta nundu kwenye shule nyingine mbali na zile za elimu maalumu.

Anasema kama elimu ni jumuisha shule zote bila kujali zina wanafunzi wahitaji , wenye uoni hafifu au wasiiona zinahitaji kuwa na vifaa vya kuwasaidia ikiwamo mashine za 'breil' pamoja na karatasi za kuchapisha maandishi hayo.

"Tunahitaji kuwa na mashine ya 'embosser' inayobadili maandishi ya kawaida kwenda mfumo wa nukta nundu," anasema Joseph.

Ni kwa sababu ili elimu jumuishi iwe na manufaa kwa wote vifaa hivyo vinatakiwa kuwapo maktaba na popote alipo mwenye uhitaji ili kila mmoja avitumie kujielimisha.

Anasema wanafunzi wengi hasa ambao wako vijijini kusikokuwa na umeme wa kutosha wanaolazimika kusoma na tochi zikiwamo za simu au za betrii na kuonya kuwa wanahatarisha afya ya macho.

"Kusoma na tochi muda mrefu , hata vibatari athari zake kwa macho yetu ni kubwa.Tunaomba serikali ianzishe utaratibu wa waganga wa wilaya na wataalamu wa macho kutembelea shule na kuchunguza wanafunzi macho maana tatizo ni kubwa."

**WALIMU WAMSIFU**

Mwalimu wa Taaluma wa Tusiime Sekondari, John Kishefu, anamwelezea Joseph akisema:"Ni mwanafunzi mwenye bidii sana. Anasema anastahili msaada wa kila hali na kwamba tangu akiwa kidato cha nne na mpaka sasa yuko kidato cha tano anaongoza katika darasa lake kwa taaluma, nidhamu na ni mfano wa kuigwa. "

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# TAKUKURU yakunjua makucha wala rushwa ngono miaka 20 jela

SAUTI za kupinga rushwa ya ngono kwa wanafunzi na wasichana, zinaendelea kusikika na kupazwa kwa nguvu na hivi karibu zimepewa msisitizo kwenye kilele cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, zilizohitimishwa wiki iliyopita, wadau wakitaka ukomeshwe.

Aidha, umma unakumbushwa usichukulie poa kwa kuwa kosa la rushwa ya ngono linabeba mashtaka ya uhujumu uchumi na adhabu kwa anayepatikana na hatia inaweza kuwa kifungo cha miaka 20 jela.

Ni mambo yanayoibuka hivi karibuni jijini Dar es Salaam, katika mkutano wa tathmini ya kampeni ziitwazo 'safari salama bila rushwa ya ngono'.

Washiriki wanataka juhudi zaidi ikiwamo kutoa elimu inayobainisha madhara ya rushwa ya ngono iwafikie wengi kuanzia kwenye vijiwe vya bodaboda, madereva mbalimbali wakiwamo daladala, wafanyabiashara sokoni hadi shuleni ili kuwalinda wanafunzi wafanikiwe katika elimu.

UHUJUMU UCHUMI

Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma, kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Temeke, Esther Mkokota, anasema, kupitia marekebisho ya Sheria namba 3 ya mwaka 2016, Sheria ya Uhujumu Uchumi ilifanyiwa mabadiliko.

Anasema, hivyo inatambua makosa yote yaliyopo ndani ya sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, isipokuwa kosa chini ya kifungu cha 15 ni makosa ya uhujumu uchumi.

Na kwamba rushwa ya ngono sasa ni kosa la uhujumu uchumi na adhabu yake si faini tena, ila ni kifungo cha miaka hadi 20 jela.

Anasema, kwa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007 imetamka kosa hilo chini ya kifungu cha 25, ambapo kwa tafsiri isiyo rasmi kifungu hicho kinasema: "Mtu yeyote ambaye kwa kutumia nafasi yake au mamlaka yake katika kutekeleza majukumu yake anadai au analazimisha upendeleo wa kingono au upendeleo mwingine wowote kama kigezo cha kutoa ajira, kupandisha cheo, kutoa haki au upendeleo wowote unaotambulika kisheria atakuwa ametenda kosa."

Anafafanua kuwa sheria hiyo inawahusu pia madereva wa bodaboda, bajaj, daladala na wengine ambao wanatumia nafasi zao kuwarubuni wanafunzi kwa lifti na kisha kufanya nao ngono.

Anakumbusha kuwa rushwa ya ngono inahatarisha maisha ya mtu na kudhalilisha utu lakini pia inamharibia mwanafunzi ndoto zake za baadaye katika elimu, hivyo wote waungane kuitokomeza.



Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma TAKUKURU Mkoa wa Temeke, Esther Mkokota (kushoto), akitoa somo la rushwa ya ngono. Kulia ni Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, Mshauri wa Kitaalam wa Mfuko wa Wanawake Tanzania, Dk. Dinah Mmbaga na Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni, Rose Mayala. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

Aidha, Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma, TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni, Rose Mayala, anasema, kuanzia shule za msingi hadi vyuoni, kuna klabu za kupambana na rushwa ya ngono.

"Wanafunzi watumie klabu hizo kutoa taarifa kwetu za vitendo hivyo ili nasi tuandae mtego wa kunasa watuhumiwa kwa lengo la kukomesha vitendo hivyo vinavyowaharibia watoto wa kike malengo yao," anasema Mayala.

Wakitoa maoni wadau wanaopinga rushwa ya ngono, ambao waandaaji wake ni asasi ya kiraia ya Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), waliowaalika madereva mbalimbali wakiwamo wa bodaboda, bajaj, daladala, walimu na viongozi wa dini, TAKUKURU, maofisa wa ustawi wa jamii wazazi na wazazi.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, anasema, vita ya rushwa ya ngono kwa wanafunzi na wasichana aliianza tangu mwaka 2018 kwa kushirikisha na baadhi ya madereva wa bodaboda, bajaj na daladala.

"Tulifanya hivyo, kwa sababu ni miongoni mwa wanaotuhumiwa kuwarubuni wanafunzi kwa lifti na tangu wakati huo, kuna mafanikio, kwani baadhi yao sasa ni mabalozi wa vita ya rushwa ya ngono," anasema Mawinza.

Anaeleza kuwa WAJIKI inafanya kazi wilaya za Temeke, Kinondoni na Ilala na ina madereva waliopata elimu ya kulinda wanafunzi dhidi ya rushwa ya ngono na wanaendelea kuisambaza kwa wengine.

"Si kwamba tumemaliza tatizo, bali kwa kiasi fulani, juhudi zimefanyika za kukabiliana na vitendo hivyo na bado tunaendelea nazo na tunaomba wadau zaidi mtuunge mkono," anasema.

Dereva wa bodaboda eneo la Mwananyamala, Godbless Kayombo, anasema, tangu apate elimu kutoka WAJIKI, amekuwa msaada mkubwa kwa wenzake, na kwamba kwenye kijiwe chao hakuna dereva anayewarubuni wanafunzi.

**TAHADHARI KWA MABINTI**

"Pamoja na hayo, niwaombe wanafunzi wasichana wasijenge mazingira yanayosababisha udhalilishaji," anasema Kayombo.

Anaungwa mkono na kiongozi wa dini, Mohamed Chunga wa Makumbusho, anayewataka watoto wa kike wajiheshimu na kujiamini kwa kuzingatia uvaaji wa mavazi bora ili wawe salama zaidi.

Mwenyekiti wa madereva wa daladala yanayotoka Makumbusho hadi Posta, Festo Kibasa, anasema, kila mzazi na mlezi anatakiwa kutambua kuwa mtoto wa mwenzake ni wake pia, hivyo amlinde dhidi ya rushwa ya ngono.

"Katika eneo langu la kazi, kwa sasa siyo rahisi kukuta wanafunzi wakizagaa ovyo ni lazima nijue ni kwa nini na ninawapandisha katika daladala wawahi shule ama nyumbani ili waepuke vishawishi," anasema Kibasa.

Anagrace Titus, anatoa elimu ya madhara ya rushwa ya ngono, katika machinjio ya ng'ombe Gongo la Mboto, na anataka vita hiyo isiishie kwa wanafunzi na wasichana bali iwafikie watu wazima.

"Kule kwenye machinjio ya ng'ombe, wanawake wanapewa nyama bure na kisha wanatoa ngono kwa wazuzaji, hayo wanayasema wazi, kwa hiyo hao nao wanatakiwa kuelimishwa," anasema Anagrace.

**MIKAKATI YA MWAKA 2021**

Baada ya majadiliano ya kutwa nzima, wadau hao wanaweka mikakati ya kufanikisha vita hiyo kwa mwaka ujao ambayo miongoni mwake ni kutoa elimu kwa wahusika wakiwamo madereva wa vyombo mbalimbali, sokoni na sehemu nyingine za huduma ili wahusika watambue umuhimu wa kumlinda mtoto wa kike na hasa wanafunzi ambao wamekuwa ni waathirika wakubwa wa ukatili huo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Makumbusho, Pelagia Mdimi, anasema, si huko tu bali hata nyumba kwa nyumba, ili jamii ijue wajibu wa kuwalimda watoto wa kike wasiendelee kukumbana na rushwa ya ngono.

"Lakini pia mwaka ujao ni muhimu wanafunzi wajengewe ujasiri wa kupaza sauti ili wasinyamaze wanapofanyiwa vitendo hivyo, na viongozi wakiwamo wa dini wanatakiwa kuhusika zaidi," anasema Mdimi



Baadhi ya washiriki wa tathmini ya kampeni za Safari salama bila rushwa ya ngono wakifuatilia maelezo kutoka kwa wataalam (hawapo pichani).

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# 'Tamu, chungu' za sheria vikwazo ulinzi mazingira

USIMAMIZI endelevu wa mazingira, pamoja na mambo kama misitu unasisitiza ushiriki wa watu katika ngazi zote za maamuzi hasa kwenye masuala yanayoathiri mazingira yao.

Ni kwa sababu watu ndiyo chanzo cha mamlaka yote ya serikali, kwa mujibu wa ibara ya 8(1),(a) ya katiba ya Tanzania ya 1977.

Kwa hiyo ushiriki wao ni zaidi ya kuzungumza na kusikilizwa bali pia kushirikiana na serikali kwenye kuibua masuala, kuainisha vipaumbele, kupendekeza mpango kazi, suluhisho na pia namna bora ya matumizi ya rasilimali na uwajibikaji katika utekelezaji.

Mwanasheria wa Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), Clay Mwaifwani, anasema ushiriki wa watu hauiondoi serikali kwenye nafasi yake kama mfanya maamuzi ila unaileta karibu na watu na kuwapa umiliki wa maamuzi na mabadailiko.

Ushiriki wa wananchi huongeza uhalali na kukubalika kwa serikali na mipango yake kwa sababu ustawi wa watu ni kipaumbele cha maamuzi yote ya serikali.

"Vivyo hivyo kwenye usimamizi wa mazingira, serikali inawajibika kuhakikisha mazingira yanatunzwa na kusimamiwa lakini pia kuwezesha uzalishaji bila kuathiri vizazi vya sasa na vijavyo." Anaongeza.

Anasema yanapofanyika maamuzi yanayoweza kuathiri mazingira, serikali inatakiwa kuhakikisha watu wanashiriki kikamilifu katika mchakato wa kufikia maamuzi hayo, anasema.

Kanuni ya 10 ya Tamko la Rio la Mazingira na Maendeleo la mwaka 1992 inaeleza kuwa masuala yote ya mazingira yatatekelezwa kwa ufanisi na yatakuwa yenye matokeo chanya iwapo yatafanywa kwa kumshirikisha kila mmoja.

"Ushiriki wa watu unakamilika iwapo watu wote wanaweza kupata taarifa zote muhimu zihusuzo mazingira."

Tamko hilo limefanywa msingi wa sheria za usimamizi na uhifadhi wa mazingira na maliasili sehemu nyingi duniani, ikiwemo Tanzania.

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kifungu cha 178 inaeleza kuwa watu watakuwa na haki ya kupewa taarifa kwa wakati kuhusiana na mpango wowote wa kiutawala unaoweza kuathiri mazingira yao na pia watakuwa na haki ya kushiriki katika mchakato wa maamuzi.

Sheria hiyo inataja baadhi ya mambo ambayo watu watashirikishwa katika ngazi zote za maamuzi kuwa ni maandalizi, utungwaji wa sera za mazingira, mikakati, mipango, sheria na kanuni zinazosimamia uhifadhi wake.

Ushiriki wa watu kwenye usimamizi wa mazingira na maliasili unaweza kufanywa kwa ufanisi zaidi katika ngazi za chini za utawala kama serikali za mitaa na za vijiji. Mikutano ya serikali ya vijiji ama mitaa ni jukwaa linalohakikisha ushiriki wao kwenye usimamizi wa mazingira na maliasili.



Mwanasheria wa LEAT, Clay Mwaifwani. **PICHA: LEAT.**

Kuwapo kwa sheria yenye kueleza utaratibu unaopaswa kufuatwa ili kuwezesha ushiriki wa watu ni jambo moja ilihali ushiriki kamilifu wa watu ni jambo jingine, anasema Mwanasheria Baraka Thomas kutoka LEAT, kwamba ushiriki wao hauishii kwenye sheria ya mazingira ya 2004, bali unahusisha nyingine zote zinazohusu usimamizi wa rasilimali.

Misitu ni rasilimali mojawapo inayosimamiwa na kulindwa na sheria na katiba ambayo inaanzisha mamlaka ya serikali za mitaa na ibara ya 146 ya katiba hiyo inaeleza kuwa madhumuni ya kuanzishwa kwa mamlaka hizo ni kupeleka madaraka kwa wananchi.

Misitu iliyoko kwenye ardhi ya vijijini inasimamiwa na vijiji na mamlaka ya juu ya uongozi wa vijiji ni mkutano mkuu wa kijiji.

Thomas anasema licha ya ukweli kuwa wanavijiji ndiyo walinzi wa misitu, uamuzi wa kuvuna au kutoivuna hufanywa na ofisa misitu wa wilaya.

Anaeleza kua mfumo wa utendaji wa namna hiyo unawapa wanavijiji haki ya kushiriki usimamizi wa mazingira na rasilimali kwa mkono mmoja na kuwapora haki hiyo kwa mkono mwingine.

> " Kwa mfano utungwaji wa sheria kwa hati ya dharura. Hati ya dharura ni jambo halali lililowekwa kisheria na litafaa iwapo litatumika kwenye mambo ya dharura." Anasema Thomas.

Mbali na kutoa haki na kuipora, sheria zina mianya mingi inayowanyima watu haki ya kushiriki kikamilifu kusimamizi wa mazingira na rasilimali zao.

" Kwa mfano utungwaji wa sheria kwa hati ya dharura. Hati ya dharura ni jambo halali lililowekwa kisheria na litafaa iwapo litatumika kwenye mambo ya dharura." Anasema Thomas.

Mambo mbalimbali yanayofanyika wakati wa utungwaji wa sheria kwa hati ya dharura huwanyima watu nafasi ya kushiriki kikamilifu katika utungwaji wa sheria hivyo kwenda kinyume na dhana ya ushirikishwaji wananchi.

Anataja sheria zilizotungwa kwa hati ya dharura ikiwamo ya Umiliki wa Milele wa Utajiri wa Taifa na Raslimali za Maliasili ya mwaka 2017 (Sheria namba 5 ya mwaka 2017)

Anasema kupatikana kwa sheria kwa hati ya dharura, kunawakosesha watu nafasi ya kushiriki na kuamua kikamilifu hatma ya mazingira na rasilimali za maliasili na pia wawakilishi wao wanakosa nafasi ya kufanya mijadala na kurudi majimboni kufanya mikutano na watu na kuchukua maoni yao ili kuyafikisha bungeni.

Mbali na watu kukosa nafasi ya kufanya maamuzi kwenye sheria zinazotungwa kwa hati ya dharura, kuna changamoto nyingine nyingi zinazowakosesha nafasi ya ushiriki mojawapo ikiwa ni kukosekana kwa mindombinu wezeshi ili kutimiza matakwa ya kisheria juu ya ushirikishwaji.

Anasema sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, kifungu cha 178(5),(a) inaeleza kuwa Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) litakuwa na wajibu wa kuandaa midahalo mbalimbali ili kupata maoni ya watu.

Thomas, anahoji: "Je, kuna mazingira rafiki ya kuwezesha midahalo nchi nzima ilihali sheria zenye kuhifadhi mazingira na maliasili zinatungwa kwa hati ya dharura?"

Sheria inaeleza kuwa watu watakuwa na haki ya kupata taarifa mapema kuhusu kuandaa sera au kutunga sheria, lengo likiwa kuwapa muda wa kutafakari na kuandaa maoni yao.

"Swali muda wa kutafakari nia ya serikali na kupitia taarifa muhimu uko wapi ilihali sheria inakwenda bungeni kwa hati ya dharura?"

Mbali na hayo, hoja nyingine inatyohitaji majibu na pengine majibu ya swali hilo yatatosha kujibu na maswali ya awali ni je, tunatunga sheria zenye kusimamia mambo muhimu kwa taifa kwa hati ya dharura kwa haraka ipi? Tunakimbilia wapi?, anahoji mwanasheria huyo.

Nakumbusha kuwa usimamizi bora wa mazingira unaweza utafanyika kwa maslahi ya watu na namna bora ya kuyafikia maslahi ya wananchi ni kuwapa umiliki wa mchakato , kuanzia ushiriki unaohama kutoka kwenye maandishi ya kisheria na kuwa dhahiri tena kwa kutekelezwa.

Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT) inaamini kuwa ustawi wa leo na karne zijazo wa Tanzania upo kwenye usimamizi endelevu wa mazingira na raslimali za nchi.

LEAT inasisitiza ushiriki wa wananchi kufanya maamuzi yanayoweza kuathiri mazingira pamoja na rasilimali zao.

Taasisi hiyo inasema ni lazima ushiriki kamilifu, uwape watu na wawakilishi wao muda wa kutosha kutafakari, kuandaa hoja, kutoa maoni kwenye mijadala na midahalo mbalimbali na kuipa serikali nafasisi ya kupokea maoni, kuchambua , kuyafanyia kazi na ya kuacha na kutoa sababu za kuyaweka pembeni.

LEAT inakumbusha usemi kuwa weledi wa taifa utapimwa kwa namna linavyoyasimamia mazingira yake, hivyo wote wana wajibu wa kuyatunza na hayo yatatekelezeka kutakuwa na ushiriki wa wadau wote.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

### VITA UJAUZITO

# RPC, hakimu ni majemedari wapya mapambano shuleni

KESI za mimba za wanafunzi mkoani Shinyanga zinaendelea kuwa 'mwiba', huku watuhumiwa na washitakiwa wanaowapatia ujauzito mara nyingi kesi zao zikiishia njiani.

Baada ya hapo ni kuachiwa huru bila ya hukumu kutokana na ukosefu wa ushahidi hali inayowalinda walalamikiwa.

Shinyanga unaongoza kitaifa kwenye matukio ya mimba za utotoni kwa asilimia 59, kwa mujibu wa takwimu za kitaifa zilizotolewa mwaka (2012), ikifuatiwa na Tabora 58, na ya tatu ni Mara asilimia 55.

Kamanda wa Polisi wa mkoa Debora Magiligimba, anasema tatizo la ukosefu wa ushahidi wa kesi za mimba za wanafunzi, limekuwa kichocheo kikubwa cha matukio hayo kuendelea.

Ndiyo sababu ya watuhumiwa na washitakiwa kukwepa adhabu na kurudi uraiani kuendeleza udhalilishaji, anasema.

Wanafunzi wanapohojiwa kuhusu waliowapatia ujauzito na kuandika maelezo polisi, huwataja na tunakwenda kuwakamata, lakini wanaporudi nyumbani hurubuniwa na wazazi na kumkana mtu huyo na hatimaye ushahidi huharibika.

Anasema asilimia kubwa ya matukio hayo ya ukatili dhidi ya watoto zikiwamo mimba za wanafunzi, yanafanywa na ndugu na jamaa wa karibu na familia, ndiyo maana wazazi hupenda kuitana pembeni na kumaliza kimya kimya kwa kupeana fedha ama mifugo na kisha kuharibu ushahidi ili mtuhumiwa awe huru.

"Mfano kesi zimeshafikishwa polisi zinazohusu ukatili dhidi ya watoto zikiwamo mimba za wanafunzi, nyingi zinawahusisha jamaa wa karibu wa wanaposhindana kwenye malipo ndipo tunawaona polisi, lakini wakishamalizana na mtuhumiwa kuachiwa huru hatuwasikii,"anasema Magiligimba.

"Ndicho kinachofanyika mtoto huyo akirudi polisi kuweka sawa ushahidi anamkana aliyemdhalilisha kuwa hamjui, wala hamtambui mtu aliyempatia ujauzito na maelezo aliyoyatoa hapo awali siyo yake na huacha kuhudhuria mahakamani. Tena wapo wanaotoroshwa na wazazi kwenda mikoa mingine na ndiyo mwisho wa kesi," anaongeza Kamanda.

Aidha anataja takwimu za matukio ya kesi za ukatili dhidi ya watoto zikiwamo mimba za wanafunzi, kuwa mwaka huu kuanzia June hadi Agosti yameripotiwa matukio 231, wakati 2019 kwa kipindi kama hicho yalitokea 151 sawa na ongezeko la matukio 80.



Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Shinyanga, Mary Mrio. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**




Kamanda Debora Magiligimba, akizungumza kwenye uzinduzi wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia mkoani Shinyanga.

Victoria Maro ni Mkuu wa Dawati la Jinsia Polisi Mkoa wa Shinyanga, anaelezea kuwa kesi za ukatili dhidi ya watoto zilizofungwa lakini kutokana na kukosa mwendelezo ni 70.

Hakimu Mkazi Mfawidhi Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani Shinyanga Mary Mrio, anasema tatizo linalosababisha matukio ya mimba za wanafunzi mkoani ni kuleana, na kubainisha tangu amefika mkoani Shinyanga kufanya kazi ana miezi mitatu sasa, lakini ameshangaa kukuta kesi na namna hiyo zikiwa zimefutwa sababu hazina ushahidi.

Anasema alipofanya kazi mkoani Simiyu hakuna cha kesi kufutwa sababu za ushahidi kwani alikuwa akiagiza kukamatwa wazazi na walezi wa waathirika na kuwabana hatua iliyoondoa kufanya makubaliano na upande wa mtuhumiwa kwa lengo la kumaliza kesi kimya kimya.

"Kesi hizi za matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto kuzisikiliza zinachukua wiki mbili tu au siku kadhaa unatoa hukumu na sheria ikifuata mkondo wake na kisheria inaelekezwa mwisho miezi sita kesi iwe imeshakwisha, lakini nilivyokuja hapa Shinyanga naona kesi zinachezewa tu. Kwangu nitawafunga sana jela,"anasema Mrio.

"Ninachoomba kuwapo na ushirikiano wa kutosha, mtuhumiwa akikamatwa wa matukio ya mimba za wanafunzi, nipigieni simu hata usiku wa manane nitaamka na kufanya kazi usiku huo huo na hata kama akikimbia hukumu itamkuta huko huko, akikamatwa ni jela," ameongeza.

Aidha, anasema atatoa maagizo kwa mahakimu wote mkoani Shinyanga kuanzia za mwanzo, hakuna kucheza na kesi za mimba za wanafunzi wala kukaa nazo muda mrefu na kusababisha waathirika kumkana mtuhumiwa sababu ya wazazi kumalizana kimya kimya.

Mrio anaeleza kuwa hapendi kusikia kesi ya mimba za wanafunzi inafutwa.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anaeleza kusikitishwa na wazazi ambao wamekuwa wakimaliza kesi kienyeji kitendo ambacho kimekuwa kikisababisha matukio hayo kuendelea, sababu ya washitakiwa hawafungwi jela na kuona kama kamchezo.

Anatoa maagizo kwa watendaji serikali kuanzia ngazi ya kijiji, kudhibiti matukio hayo ya mimba na ndoa za utotoni, pamoja na kuwachukulia hatua wazazi ambao wamekuwa wakimaliza kesi kimya kimya, na kuwarubuni watoto kuwakana watuhumiwa na kusababisha kuachiwa huru.

"Nawaomba sana wazazi tuungane kwa pamoja kupambana kutokomeza matukio ya mimba na ndoa za utotoni, sababu yanakatisha ndoto za wanafunzi na kuwafanya waishi maisha magumu na kuanza kulea watoto wenzao huku wakiwa hawana uelekeo wa maisha wala hatma ,"anaonya Mboneko.

Mussa Ngangala ni Mkurugenzi wa Shirika la (TVMC) mkoani Shinyanga, linajishughulisha na kutetea haki za watoto, anasema mara baada ya kuona tatizo la kumaliza mambo kimya linaendelea wamepanga kujenga nyumba salama, ambayo itakuwa ikihifadhi waathirika wa mimba za utotoni ili wasirudi nyumbani na kurubuniwa kuwakana washtakiwa na kuharibu ushahidi.

Anasema tatizo ambalo linasababisha matukio haya ya mimba za wanafunzi kuendelea ni jamii kuendekeza mila na desturi kandamizi kwa watoto wakike, ambapo kesi hizo wanazigeuza kama vitega uchumi vya familia, wakishapata fedha au mifugo hawafuatilii wala kushirikiana na polisi kuwafikisha wahusika mahakamani.

Anasema watuhumiwa wakianza kufungwa jela, matukio hayo mimba za wanafunzi yatabaki historia mkoani Shinyanga, sababu watu watakuwa wakiogopa kwenda jela, na kuacha kuhadaa wanafunzi .

Mzee mashuhuri mkoani Shinyanga, Sospeter Swagi mkazi wa Ibadakuli, anasema jamii inatakiwa kupewa elimu ya kutosha juu ya madhara ya kurubuni wanafunzi na kufanya ngono katika umri mdogo.

Anasema baadhi ya makabila hasa ya kanda ya ziwa, mtoto wa kike akianza kupevuka hakai nyumbani na ana tambulika kuwa ameshakua na anapaswa kuolewa bila ya kujali ni mwanafunzi au mdogo.

Lengo ni wazazi wake wapate fedha ama mifugo na hawajui madhara mbali na kuangalia mali tu.

"Tatizo la kumaliza kesi kimya kimya na kuharibu ushahidi, ni jamii kuoneana huruma na kuogopa uhasama baina ya ukoo fulani au kuvunja undugu. Ndiyo maana kesi nyingi za mimba za wanafunzi huishia njiani na kukosa uelekeo sababu ya ushahidi kukosekana mahakamani,"anasema Swagi.

Mwenyekiti wa Baraza la Watoto mjini Shinyanga Victoria Deogratius, anaiomba serikali kukomesha matukio ya mimba na ndoa za utotoni sababu yamekuwa tatizo lisilokwisha.



# China yasaidia taulo kike za mil. 80/-

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

UBALOZI wa China nchini kupitia taasisi ya Agri Thamani umetoa msaada wa taulo za kike kwa wanafunzi wa shule ya sekondari Bwaga wilayani Kongowa wenye thamani ya Sh. milioni 80 ili kusaidia kupunguza utoro kwa wanafunzi wa kike wakati wa hedhi.

Msaada huo umelenga kuwasaidia watoto 3,000 wa shule za sekondari za mikoa ya Tabora, Tanga, Lindi, Kigoma na Kagera.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo kwa wanafunzi hao, Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Neema Lugangira, alisema lengo la msaada huo ni kupunguza kero zinazowakabili watoto wa kike shuleni hususani wanapokuwa kwenye kipindi cha hedhi.

**Hizi taulo ni muhimu sana kwa wanafunzi wa shule, kwa sababu zinawasaidia kuhudhuria darasani hata wanapokuwa katika kipindi cha hedhi.**

"Hizi taulo ni muhimu sana kwa wanafunzi wa shule, kwa sababu zinawasaidia kuhudhuria darasani hata wanapokuwa katika kipindi cha hedhi," alisema Lugangira

Lugangira, ambaye pia ni Mbunge wa viti maalumu anayewakilisha mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO), alisema moja ya majukumu ya taasisi hiyo ni kuhakikisha wanafunzi na jamii kwa ujumla inaondokana na kero zinazowakabili watoto wa kike.

Alifafanua kuwa katika utekelezaji wa mradi huo fedha hizo zimesaidia kupatikana taulo za kike ambazo kila mwanafunzi atapata taulo za kutumia ndani ya mwaka mzima.

Alisema wanafunzi wengi wanashindwa kuhudhuria shuleni wanapokuwa kwenye hedhi kwa sababu ya kukosa taulo za kike, ambazo huwasaidia kujistiri wanapokuwa katika hali hiyo.

"Kwenye shule hii ya Bwaga tumeanza kutoa taulo 95 lakini tutawafikia wanafunzi wote... na hii ni baada ya shule kufunguliwa tunajua watakuwapo wa kidato cha tatu na cha kwanza, na nyingine tutazifikisha kwenye mikoa mingine," alisema Lugangira.

Balozi wa China nchini, Wang Ke, alisema ili kuunga mkono juhudi za Serikali katika utoaji wa elimu bila malipo watatoa ufadhili kwa wanafunzi kusomeshwa China. Balozi Wang alisema fursa hiyo ni utekelezaji wa makubaliano kati ya Ubalozi na Taasisi ya Agri Thamani ambayo itaanza kwa wanafunzi watakaomaliza kidato cha sita mwakani kutoa mikoa ya Dodoma na Kagera.

Alisema wanafunzi wa kike wanaosoma masomo ya sayansi watakaokuwa na ufaulu wa juu watapa fursa ya kufadhiliwa kusoma shahada nchini humo.

"Wanafunzi wa kike naomba mjitahidi kusoma kwa bidii kwani kuna ufadhali kwa ajili ya wale watakaokuwa na ufaulu wa juu, ili kuongeza motisha katika hili, tutaanza na wanafunzi waliopo kidato cha sita mwaka huu," alisema Balozi Wang

Kuhusu taulo za kike, Balozi Wang alisema zitasaidia kupunguza utoro kwa wanafunzi na kuongeza mahudhurio darasani pamoja na kutatua changamoto nyingine.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Rose Michael, aliishukuru taasisi hiyo kwa msaada waliopatiwa huku akiahidi kuwa watatumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

Hata hivyo, alisema kuwa wanakabiliwa na ukosefu wa chumba maalumu kwa wajili ya wanafunzi wa kike kujisitiri wanapokuwa katika hedhi.

## Mradi wawezesha maelfu wasichana kutoka kaya maskini

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

WASICHANA 3,183 kutoka kaya maskini wilayani Kongwa mkoani Dodoma wamewezeshwa kupitia mradi wa Timiza Malengo kwa Mabinti Balehe na Wanawake vijana unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF).

Mratibu wa Tasaf Wilaya ya Kongwa, Unambwe Erasto, alisema hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya mpango huo.

Alisema jumla ya mabinti hao kutoka kaya maskini Wilayani hapa wamewezeshwa na Serikali kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini unaoendeshwa na serikali kupitia TASAF.

Alibainisha kuwa mradi wa timiza malengo ulianza mwaka 2018 na unawalenga mabinti kutoka kaya maskini wenye umri wa kuanzia miaka 10 mpaka 24 wanaosoma shule na wasiosoma.

Kadhalika, alisema wanafunzi 2,040 wanaosoma shule za msingi na sekondari wanapokea Sh. 25,000 kutoka Tasaf kila mwenzi kwa ajili ya kuwasaidia kununua mahitaji ya shule.

Mratibu huyo alisema mwanafunzi akizidi umri huo anakosa sifa ya kuendelea kupokea fedha hizo kama akichaguliwa kwenda chuo kikuu ataomba mkopo wa masomo serikalini.

Alibainisha kuwa mradi huo umesaidia kuondoa utoro shuleni pamoja na kuleta mfanikio ya kielimu kwa watoto hao ambapo wengine wamefanikiwa kufika elimu ya vyuo vikuu

Aliongeza kuwa kwa mabinti ambao hawasomi jumla yao 1,143 wanawezeshwa mitaji ya ujasiriamali kiasi kisichozidi Sh. 400,000 kupitia andiko la mradi aliloomba TASAF.

Alisema kabla ya kupewa fedha hizo, walengwa waliwezeshwa mafunzo ya ujasiliamali na elimu ya namna ya utunzaji fedha watakazopewa ili kujikwamua kiuchumi.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Edsoni Sweti, akizungumza na Madiwani wa kata (hawapo pichani) wakati akifunga kikao chao cha kwanza cha Baraza la Madiwani baada ya kuapishwa, kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Keneth Yindi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Yawekea wawekezaji mazingira rafiki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Josephat Maganga, amesema mkoa wa Dodoma unaendelea kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa wawekezaji kuwekeza katika maeneo mbalimbali ikiwa ni sehemu ya kutekeleza agizo la Rais John Magufuli.

Mkuu huyo wa Wilaya, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizundua maduka ya GSM ya nguo na samani za maofisi na majumbani

Maganga, alisema serikali hivi sasa imeondoa urasimu pamoja na milolongo mirefu kwa wawekezaji ili kuwezesha upatikanaji wa vibali kuchukua muda mfupi kama ambavyo Rais aliagiza wakati akizindua Bunge la 12.

"Tunaamini kuwa kufanikiwa kwa wawekezaji ni mafanikio ya Taifa kwa ujumla ni matumaini yetu pamoja kuwa GSM mmewekeza jijini Dodoma pia mtawekeza katika maeneo mengine nchini", alisema Maganga

Pia, alisema GSM, wamefanya uwekezaji huo katika kipindi mwafaka kwani jiji la Dodoma lilikuwa linahitaji huduma hizo kwa muda mrefu.

"Uwapo wenu hapa na bidhaa hizi ni jambo sahihi ambalo mmeamua kwani huduma za samani kwajili ya mahitaji ya ofisi na majumbani tulikuwa tunalazimika kuzifuata jiji Dar es Salaam," alieleza Maganga.

Aidha, alitoa wito kwa wawekezaji kujitokeza kuwekeza jijini Dodoma kwani bado yapo mahitaji mengi.

Alisema jiji la Dodoma bado linayo ardhi ya kutosha kwa ajili ya kuwekeza huduma mbalimbali kama sekta ya afya, elimu, miundombinu pamoja na viwanda.

"Lakini serikali yetu hivi sasa imewekeza katika miradi mikubwa ambayo ikikamilika itasaidia wawekezaji kuendesha shughuli zao na hivi karibu uwanja wetu wa ndege tuliufanyia marekebisho makubwa sana ambapo hivi sasa hata ndege aina ya Air Bus inaweza kutua hapa," alisema.

Mtendaji mkuu wa GSM, Fatma Abdallah, alisema kuwa anampongeza Rais Magufuli kwa kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji.

Alisema hali hiyo itasaidia kuongeza wawekezaji wengi kutokana na mazingira rafiki yaliyopo ikiwemo agizo la rais kutaka vibali vya wawekezaji kutolewa ndani ya siku 14.

"Pamoja na kuwekeza katika maduka haya ya nguo na samani, lakini pia GSM tutaendelea kuwekeza katika sekta za kiuchumi na kijamii", alisema Abdallah



# Watuhumiwa kuuza shamba, kugawanya fedha

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

VIONGOZI wa Kijiji cha Kambikatoto katika Wilaya ya Chunya, wanatuhumiwa kushirikiana kuuza shamba la kijiji hicho lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 11,000 na kisha kugawana nusu ya fedha hizo za mauzo hayo.

Aidha wanatuhumiwa kushirikiana na ndugu zao kugawana ardhi yenye ukubwa wa ekari 1,480, huku wakisimamia uuzwaji wa viwanja hewa, hali ambayo imesababisha wananchi kupoteza fedha nyingi.

Kufuatia hali hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Saimon, ameusimamisha uongozi wa kijiji hicho akiwamo Ofisa Mtendaji na Ofisa Ugani kuunda kamatie huru ya kwenda kuchunguza sakata hilo. Mayeka alifanya uamuzi huo kwenye mkutano wa hadhara wa Kijiji hicho, ambapo alisema endapo kamati hiyo itabaini uwapo wa jinai viongozi hao watachukuliwa hatua za kisheria na kiutumishi ikiwamo kufukuzwa kazi.

Aliwataka wananchi wote ambao waliuziwa viwanja na viongozi hao kwenda kudai fedha hizo ili warudishiwe, huku akizuia viongozi hao pamoja na ndugu zao kuendelea kuyatumia mashamba ambayo waligawana kinyume cha utaratibu.

**Mashamba hayo walikuwa wanayatumia kwa ajili ya kulima, na kwamba kwa sasa wanashindwa kuyatumia kwa sababu ya mgogoro na wanakijiji wenzao.**

"Yale mashamba ambayo waligawana nimewanyang'anya, hawana hata ekari moja, kama kuna shamba waliuza basi wewe uliyeuziwa nenda kadai fedha zako na ikiwezekana nenda mahakamani, mimi niko tayari kuwa shahidi wako," alisema Mayeka.

Alisema endapo uchunguzi wa kamati aliyoiunda utabaini kuwa mashamba hayo waliyapata kihalali, watarejeshewa, huku akiwataka wananchi kuwa watulivu wakati uchunguzi huo unafanyika pamoja na kutoa ushirikiano kwa kamati hiyo. Kabla ya kutoa uamuzi huo, Mkuu wa Wilaya alitoa nafasi kwa wananchi waliokuwa wanawalalamikia viongozi hao kueleza kilichotokea, ambapo walidai kuwa waliuziwa viwanja hewa chini ya usimamizi wa viongozi wao.

Majaliwa Shija, alisema aliuziwa shamba lenye ukubwa wa ekari 40 kwa gharama ya sh. milioni 1.05 na kwamba mmiliki halali wa shamba hilo alikuwa hafahamiki. Alisema baada ya muda wananchi walianza kulalamika wakidai shamba hilo lilikuwa mali ya kijiji, hivyo wakawa wanadai kuwa hawakushirikishwa wakati wa kuuzwa kwa shamba.

"Mimi nilianza kupata wasiwasi na kila nikijaribu kuwafuatilia viongozi hawa walikuwa hawatoi majibu yanayoeleweka, tunakuomba Mkuu wa Wilaya utusaidie ili ikiwezekana waturudishie fedha zetu au tumilikishwe mashamba haya," alisema Shija.

Naye Makoye Ng'umbi, alisema pamoja na kwamba waliuziwa mashamba hayo na viongozi wa kijiji, lakini hawakuandikishana popote kutokana na viongozi hao kuwazungusha kuwapa vielelezo vya kuuziwa.

Alisema mashamba hayo walikuwa wanayatumia kwa ajili ya kulima, na kwamba kwa sasa wanashindwa kuyatumia kwa sababu ya mgogoro na wanakijiji wenzao.

Aliiomba Serikali kuingilia kati kutatua mgogoro huo ambao alidai unawanyima usingizi kutokana na kuwa na hofu ya kupoteza fedha zao.



Baadhi ya wananchi wa Kitongoji cha Mwashikamile katika Kijiji cha Yara, wilayani Mbarali, Mkoa wa Mbeya, wakishirikiana kuvusha pikipiki kwenye daraja la miti lililopo kwenye mfereji wa maji wa Skimu ya umwagiliaji ya Shamba la Mwekezaji la Kapunga ambapo wanadai kuzuiliwa kujenga daraja la kisasa na mwekezaji wa shamba hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mbaroni madai ya kukutwa na gongo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu saba kwa tuhuma za kukutwa na pombe haramu ya moshi (gongo) pamoja na dawa za kulevya aina ya bangi katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, aliyasema hayo jana alipokuwa anazungumza na wandishi wa habari ambapo alisema watu hao walikamatwa katika matukio matano tofauti.

Kamanda Matei alisema tukio la kwanza lilitokea katika eneo la ZZK lililopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambapo, Sikujua obasi (19) alinaswa na lita tano za gongo pamoja na mtambo wa kutengenezea pombe hiyo.

Alisema kijana huyo alinaswa na Polisi Desemba 11, mwaka huu saa 6:00 mchana, na kwamba mtuhumiwa ni mtengenezaji, muuzaji na mtumiaji wa pombe hiyo.

Alisema katika tukio la pili Jeshi hilo liliwakamata Yusuph Segereti maarufu kwa jina la 'Masuba' (54), Geofrey Mwangoso (38) na Atufigwege Oscar (38) wote wakazi wa Kyimo wilayani Rungwe wakiwa na pombe haramu ya moshi lita 16.

Alisema watu hao pia ni wauzaji na watumiaji wa pombe hiyo haramu na kwamba walikamatwa Desemba 11, mwaka huu saa 7:30 mchana wakiwa wanatumia pombe hiyo.

"Lakini pia kwenye msako wetu tulifanikiwa kukamata gongo lita 40 na pikipiki aina ya Boxer yenye namba za usajili MC. 587 CLM ambayo ilikuwa imebeba gongo hiyo na mmiliki alitoroka na kutelekeza pombe hiyo pamoja na pikipiki," alisema Kamanda Matei.

# Watumiaji simu watakiwa kuhakiki namba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BARAZA la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano nchini (TCRA-CCC), limewashauri wananchi kuhakiki namba za simu ambazo zimesajiliwa kwa kutumia vitambulisho vyao bila wao kujua ili kuepuka kukumbana na mkono wa sheria.

Angalizo hilo limetolewa kwa kuwa namba zao zinaweza kutumika vibaya. Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Mary Msuya, alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya wakati wa mkutano wa kuhamasisha, kuonya na kutoa maelekezo kwa watumiaji huduma za mawasiliano hasa kuhusu fursa za kiuchumi zinazopatikana kwenye huduma za mawasiliano.

Alisema kitendo cha mtu kutumia kitambulisho cha mtu mwingine kusajili namba yake ya simu ni kosa kwa mujibu wa sheria, hivyo akawataka wananchi kuepuka kuwasaidia watu wengine kutumia vitambulisho vyao.

Alisema endapo mwananchi yeyote atabaini kuwa kuna namba ambazo zimesajiliwa kwa kutumia kitambulisho chake lakini yeye hazijui, anatakiwa kutoa taarifa kwa mtoa huduma ili namba hizo ziondolewe.

"Kila mmoja anatakiwa kuhakiki kwa kupiga namba *106# kisha fuata maelekezo, ukibaini namba hizo ni vema ukawasiliana na mtoa huduma wa mtandao husika ili namba hiyo iondolewe, watu wengi wamerahisisha, lakini ni hatari sana kwao," alisema Msuya.

Alisema endapo mmiliki wa namba hiyo ataitumia vibaya hasa kwenye tukio la uhalifu, Jeshi la Polisi linaanza kumkamata kwanza mwenye kitambulisho kilichotumika na kwamba mpaka ibainike kuwa hakuhusika anakuwa amesota.

Alisema vitendo vya watu kutumia vitambulisho vya wengine vimekuwa vikisababishwa na mawakala wa mitandao ya simu ambao sio waaminifu kwa kuchukua picha na alama za vidole mara kwa mara bila wahusika kujua.

Aidha, Msuya alisema kwa mujibu wa sheria, mtu pekee ambaye anatakiwa kusajiliwa namba kwa kutumia kitambulisho cha mtu mwingine ni mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 18 na zaidi ya miaka 12, na kwamba chini ya hapo hairuhusiwi, na kwamba anatakiwa kutumia kitambulisho cha mzazi wake.

Vilevile, alisema baada ya mtoto huyo kufikisha miaka 18, mzazi anatakiwa kumpatia kitambulisho chake na taarifa za usajili wa simu zinabadilishwa ili zitumike za majina yake mwenyewe.

Hata hivyo, baada ya watumia huduma hasa wenye uziwi walilalamikia mfumo wa malalamiko kwenye mitandao ya simu kuwa siyo rafiki kwao kutokana na kuwa na mlolongo mrefu ambao unawafanya wasifurahie huduma.

Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Mkoa, Tusajigwe Mwalyego, alisema wanashindwa kuwasiliana na watoa huduma kuhusu matatizo ambayo wanakutana nayo kwenye mawasiliano kutokana na kutokuwapo kwa miundombinu rafiki.





# Waziri aagiza kibano watendaji bandarini

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Raisi ( Fedha na Mipango), Jamal Kassim Ali, amemuagiza Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ofisi ya Zanzibar kuwasimamisha kazi watendaji watakaoingiza mzigo kwa bei ndogo.

Alisema amebaini kuwa katika Bandari ya Malindi Mjini Zanzibar kuna mizigo ulioingizwa kwa bei ndogo kinyume cha utaratibu, jambo linaloashiria utendaji usioridhisha na viashiria vya kuvuja mapato na kuitia hasara Serikali.

Aliyasema hayo jana kwa nyakati tofauti wakati akizungumza kwenye ziara ya kuangalia utendaji wa bandari na Uiwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume akiambatana na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali.

Alisema Serikali haijaridhika na mfumo wa ukusanyaji wa mapato na kuwataka kuiboresha mifumo hiyo ili kutoa huduma bora zaidi.

Aidha, aliitaka mamlaka ya viwanja vya ndege Zanzibar kujiandaa kwa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wao ili kufanyakazi kuwa na ufanisi wakati itakapofika Desemba 31, mwaka huu, watakapokabidhiwa jengo jipya la abiria (Terminal three) ili kuleta tija kwa watumiaji.

Naye, Waziri Rahma aliwataka wafanyabiashara kulipa kodi ili Serikali ijiendeshe na kutatua matatizo ya wananchi ya sekta za elimu, afya na barabara.

"Kodi ndiyo itakayosaidia kuendesha shughuli mbalimbali ikiwamo za kijamii na kiuchumi, hivyo ni vyema kulipa kodi," alisema.

# Z'bar kuimarisha mitaala iendane na teknolojia

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

**Watajitolea kufundisha vijana wa kizanzibari ambao tayari wameshaonyesha muelekeo wa kutaka kulisaidia taifa katika utumishi wa umma uliotukuka.**

SERIKALI ya Zanzibar imesema inakusudia kuimarisha mitaala ya ufundishaji na kujifunzia ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alisema hayo juzi kwenye hafla maalum aliyoandaliwa kwa ajili yake na wanafunzi wenzake wa Chuo Kikuu cha Bradford cha Uingereza chenye tawi lake Chuo Kikuu cha Mzumbe mkoani Morogoro.

Alisema kipaumbele cha Serikali ni elimu ili baadae taifa liweze kujitegemea lenyewe kwa kuwa na wataalamu wa kutosha kwenye fani zote jambo litakalosaidia kuepuka wataalamu wa kigeni, ambao wakati mwingine wanapatikana kwa masharti yasiyotekelezeka.

Hemed alisema juhudi kubwa iliyochukuliwa na Serikali ya Zanzibar awamu iliyopita chini ya aliekua rais kwa wakati huo, Dk. Ali Mohamed Shein, katika kuimarisha sekta ya elimu itaendelezwa ili ifike wakati Zanzibar izalishe zaidi wasomi watakaokuwa na uwezo wa kuitumia taaluma yao mahali popote duniani.

Alisema washirika wa maendeleo wa ndani na nje ya Zanzibar wamekuwa wakishuhudia uharaka wa Serikali ya Zanzibar katika kipindi kifupi tokea ipokee kijiti jinsi ilivyoanza na kasi ya kuendeleza uchumi wake kwa kuondoa uzembe na kudhibiti mianya ya rushwa inadumaza maendeleo ya jamii.

Naye, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mzumbe kinachosimamia Tawi la Chuo Kikuu cha Bradford cha Uingereza, Dk. Andrew Mushi, alisema watajitolea kufundisha vijana wa kizanzibari ambao tayari wameshaonyesha muelekeo wa kutaka kulisaidia taifa katika utumishi wa umma uliotukuka.

Zanzibar imeshakuwa na vyuo vikuu vitatu ambavyo ni SUZA, ZU vilivyopo Tunguu pamoja na chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al- Sumait Chukwani ambavyo viwili kati yake vimeshafikia daraja ya kutoa wahitimu wa eimu ya Shahada ya Uzamivu ( PhD).



Baadhi ya vijana wakiwa katika kilimo cha mboga eneo la Chwaka Mkoa wa Kusini Unguja, vijana hao walikua wakifanya kazi katika hoteli za kitalii lakini baada ya kuibuka kwa corona na ajira zao kusitishwa waliwezeshwa na taasisi ya Our Farm Zanzibar iliyowapa elimu ya kilimo ili kujikomboa kiuchumi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waajiriwa hoteli waliopoteza ajira wageukia kilimo

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

BAADA ya vijana waliokuwa wameajiriwa katika hoteli za kitalii ajira zao kusitishwa kutokana na janga la Corona, wameanza kuwapa elimu ya kilimo cha mboga na matunda ili kujikwamua kiuchumi.

Akizungumza na waandishi wa habari Mwenyekiti wa Taasisi ya Our Farm Zanzibar, Taufiq Salum Turky, alisema hatua hiyo imesaidia waliokua wakitegemea mishahara kutoka kwa waajiri wao ambao ni wamiliki wa hoteli za kitalii kupata fedha kutokana na kilimo.

Turkiy aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mavuno ya nyanya, kilimo ambacho kinaendeshwa na vijana hao huko Chwaka Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema mafunzo hayo waliyatoa kwa vijana 25 ambapo hivi sasa licha ya Corona kupungua nchini, lakini bado wanaendelea na kilimo hicho.

"Kama tunavyojua Corona nchini kwetu haipo, lakini bado nchi za wenzetu ipo jambo lililopunguza idadi ya watalii wanaofika Zanzibar, ikilinganishwa na kabla ya Corona kiasi kwamba kwa sasa kuna hoteli hazina watalii kabisa,"alisema.

Aidha, alisema vijana hao licha ya kukosa mishahara katika ajira zao hali zao za kimaisha hazikutetereka sana baada ya kugeukia katika kilimo cha mboga na matunda.

Kwa mujibu wa Turkiy, malengo ya taasisi hiyo ni kuitangaza Zanzibar katika kilimo hai na vijana kupata ajira zaidi na kuacha utegemezi wa kuagiza mboga na matunda kutoka nje ya Zanzibar wakati kuna ardhi nzuri kwa ajili ya kilimo.

Alisema licha ya eneo dogo la ardhi lililopo kwa ajili ya kilimo, lakini eneo hilo likutumika kwa kulima kilimo cha kisasa kitawezesha kupata mazao mengi.

Naye, mwanzilishi wa taasisi hiyo, Ives Montel, alisema jumla ya hekari tano za mazao mbalimbali ya mboga zinazalishwa na kwamba kila baada ya miezi mitatu wanavuna ikiwamo nyanya, bilingani, pilipili hoho na ndizi.

Alieleza kuwa wataendelea kuwapati mafunzo ya kilimo vijana hasa kilimo hai ambacho hakitumii mbolea zenye kemikali.

"Mazao ambayo hayana kemikali ndio yenye soko kubwa kuliko yale yenye kemikali hivyo tutawahamasisha vijana wetu kujikita katika kilimo hai"alisema.

Akizungumza kwa niaba ya vijana wezake waliopatiwa mafunzo ya kilimo na taasisi hiyo, Ezekiel Imanuel Shayo, alisema walikuwa na hofu kubwa ya maisha baada ya kusitishwa kazi kutokana na Corona, lakini kilimo hicho kimekuwa mkombozi wao.

Alisema licha ya mafanikio mbalimbali waliyoyapata kutokana na kilimo hicho ikiwamo kupata fedha ya kujikimu, lakini wanakabiliwa na tatizo la wadudu waharibifu katika kilimo hicho ambao hushambulia mazao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

## TUNAHITAJI MAFUNDI

**TUNAHITAJI MAFUNDI WA PIKIPIKI WENYE UZOEFU, UMRI MIAKA 25-35.**
**TUMA MAOMBI KWA: linkallafrica@gmail.com**
**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI: 17/12/2020.**

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676

## MATHEMATICS TUITION.

**Mlete kijana wako** tufuatilie msingi wake wa **hisabati hadi pale shida ilipoanzia** na kuanza kuujenga tena upya. Wahusika ni kuanzia darasa la tano hadi kidato cha sita. ***Tuitions za majumbani zinapatikana pia.***

**Tupo Bunju Mwisho Dsm.**

**Simu 0655.0754 617987 na 0782 461858**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KIVUKONI KINONDONI**
**SHAURI LA MIRATHI Na. 129 LA 2020**
**Maombi ya barua ya Usimamizi wa Mirathi ya Marehemu,**
**ROGASIAN CHARLES LASWAI................ MAREHEMU**
**MATRIDA KITUNDU MLEGA................ MWOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na Haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika Jalada kama wanaona inafaa kabla ya kuletwa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya **04/01/2021.**

Hati hii imetolewa leo, **11th Mwezi 12 Mwaka 2020.**

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KIN
KINONDONI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEORGE RWEHUMBIZA NJUNWAS** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA BB** yenye namba za usajilin **T 655 BKV** chasisi namba **NCP30002289**8,yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisin taarifa**
**DAR/MAG/RB/853649/2020**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 91 LA 2020**

**ELIHURUMA THOMAS MREMI MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**TABITHA GIDEON MKUDE MDAIWA/WADAIWA**
**WITO KUITWA SHAURINI**

**TABITHA GIDEON MKUDE**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**
**ELIHURUMA T. MREMI** amefungua /wamefungua shauri la mbele ya baraza la ardhi na nyumba lililopo kinondoni (mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa **Tarehe 15/12/2020** saa **TATU** asubuhi mbele ya Mh s.WAMBILI . Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa
Imetolewa na kupigwa saini na mhuri wa baraza hii leo **Tarehe 14 Mwezi 12** mwaka **2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPHINE KOKUHABUKILWA NJUNWAS** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T 831 DUW** chasisi namba **RZH101-6011804**,yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisin taarifa**
**DAR/PHQ/RB/847546/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ASUBISYE TIMOTH MWANGOKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 454 AVG.**Chassis namba **LNJBGDE107L819412** Engine namba **B7133485.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

**Taarifa ya polisi**
**MBE/MBE/RB/854409/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISSAYA KIHICHA BIHEMO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 765 BVV LAND ROVER-DISCOVERY.** Chassis namba **SALLTGM931A712709.** Engine namba **10P04578B.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**TAARIFA YA POLISI:**
**WMB/RB/1507/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ZOLA MIC** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 0546-0165** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **PAMBA** mwaka **2012**,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa**
**DAR/KIG/RB/844899/2020**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;297/2020**

Ombi la **HELLEN FELICIAN MSABA**,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **JOSEPHAT MSABA**. Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo **Tarehe 21/12/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa **Tarehe 06/11/2020.**
**ANAOMBA TANGAZO**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

Uza,
Chenye Thamani
Kubwa Kwa Kutangaza
Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Waziri Mkuu Eswatini afariki dunia kwa corona

**Mbabane, ESWATINI**

SERIKALI ya Eswatini, imesema kuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Ambrose Dlamini amefariki dunia, wiki nne baada ya kupatikana na virusi vya corona.

Taarifa ya serikali ilisema kuwa Dlamini, mwenye umri wa miaka 52, alifariki dunia Jumapili mchana hospitalini, nchini Afrika Kusini.

Hakuna sababu ya kifo iliyotajwa, lakini hivi karibuni Dlamini alitibiwa maradhi ya Covid-19 nchini Afrika Kusini.

Dlamini amekuwa waziri mkuu wa Eswatini, nchi ambayo zamani iliitwa Swaziland.

Nchi hiyo ndogo iliyopo kusini mwa Afrika ni moja ya nchi chache ambazo bado zinatawaliwa kifalme duniani.

Nchi hiyo yenye idadi ya watu wapatao milioni moja, tayari imerekodi visa 6,768 vya virusi vya corona na vifo 127 vilivyohusishwa na corona, kwa mujibu wa wizara ya afya.

Dlamini alitangaza kuwa amepatwa na virusi vya corona Nobemba 16, Wakati huo alisema kuwa hakuwa na dalili na anahisi vyema.

Wiki chache baadaye, Desemba Mosi, serikali ya Eswatini ilisema kuwa Dlamini amehamishiwa katika hospitali ya Afrika Kusini kwa matibabu, kwa lengo la kuharakisha kupona kwake.

Juzi serikali ilisema kuwa Dlamini amefariki wakati alipokuwa akipokea matibabu katika hospitali ya Afrika Kusini, bila taarifa zaidi .

"Serikali kwa ushirikiano na familia itaendelea kulifahamisha taifa kuhusu mipango kadri inavyoendelea," Naibu Waziri Mkuu, Themba Masuku alisema katika taarifa

*BBC*




Waziri Mkuu Ambrose Dlamini, akiwa katika moja ya mikutano ya kimataifa. Serikali ya Eswatini imesema kuwa waziri huyo amefariki dunia Jumapili, ikiwa ni wiki nne tangu apatikane na virusi vya corona. **PICHA/BBJ**

# IGAD kufanya mkutano wa dharura kuhusu Tigray

**Khartoum, SUDAN**

WAZIRI Mkuu wa Sudan, amesema amekubaliana na mwenziwe wa Ethiopia kufanya mkutano wa dharura, utakaojumuisha mataifa yaliyo katika Shirikisho la Maendeleo la Pembe ya Afrika (IGAD), kuhusu utatuzi wa mzozo wa Tigray.

Hata hivyo pamoja na jitihada za Shirika la Habari la Ufaransa (AFP), upande wa pili wa ofisi ya waziri mkuu wa Ethiopia haikuweza kupatikana kutolea ufafanuzi tangazo la Waziri Mkuu wa Sudan, Abdallah Hamdok.

Mwishoni mwa wiki, Hamdok alikwenda Addis Ababa kwa lengo la kuujadli mzozo wa Tigray na Waziri Mkuu wa Abiy Ahmed.

Hamdok ni kiongozi wa kwanza wa kigeni kuitembelea Ethiopia, tangu kuzuka kwa mapigano Novemba 4, ambayo yamezusha janga la kibinadamu.

Ofisi ya Hamdok ilisema ziara hiyo inaongozwa na mazungumzo yenye tija na kwamba imekubaliwa kufanyika kwa mkutano wa dharura wa IGAD.

Shirikisho hilo lililoanzishwa mwaka 1996, linayakutanisha mataifa ya Afrika Mashariki ambayo ni Ethiopia, Sudan, Djibouti, Kenya, Somalia, Sudan Kusini na Uganda.

Maofisa wa Serikali ya Sudan waliambia AFP kwamba, mkutano wa Hamdok na Abiy umekuwa wenye tija katika hatua ya kufanyika mkutano wa dharura wa IGAD, kufufua kamati ya pamoja kushughulikia kero za katika maeneo ya mipaka.

Abiy, ambae ni mshindi wa Tuzo ya Nobel ya mwaka jana, amekuwa mkaidi dhidi ya mashinikizo ya kutaka mazungumzo ya amani ya jumuiya ya kimataifa la majuma kadhaa, yakiwamo ya Marekani, Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika.

Kwa upande wake Abiy, alisema Hamdok katika mazungumzo ya ana kwa ana alionesha uungaji mkono katika mashambulizi dhidi ya Wapiganaji wa Chama cha Ukombozi cha watu wa Tigray, TPLF na kampeni yake ya kuwapokonya silaha.

*DW*

# Bosi wa UN ziarani DRC

**Kinshasa, DRC**

NAIBU Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia operesheni za kulinda amani, Jean-Pierre Lacroix, ameanza ziara ya siku tano nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kuanzia jana.

Jean-Pierre Lacroix atakutana kwa mazungumzo na tume ya Umoja wa Mataifa nchini DRC, Monusco.

Ziara ya Lacroix, anayeshughulikia operesheni za kulinda amani nchini DRC, ilipangwa kwa wiki kadhaa na kuahirishwa kwa baada ya naibu huyo, kujiweka karantini.

Hii ni mojawapo ya ziara za kawaida za mkuu wa operesheni za kulinda amani za Umoja wa Mataifa nchini DRC.

Baada ya kuwasili nchini humo, Desemba 13, atabaki kwa siku mbili Kinshasa, kabla ya kuelekea mashariki mwa nchi, katika mikoa ya Kivu Kaskazini na Ituri.

Katika ziara yake hiyo, Jean-Pierre Lacroix atajadili na viongozi wa MONUSCO kuhusu tume hiyo, wakati muhula wake unatarajiwa kuongezwa muda Ijumaa 18 Desemba.

Jean-Pierre Lacroix pia atakutana na mashirika yasiyo ya kiserikali, baadhi ya wajumbe mashirika ya kiraia na watu waliotoroka makazi yao, wakati mabadiliko ya ujumbe wa UN.

Hayo yanajiri wakati DRC inakabiliwa na mzozo wa ndani kati ya muungano wa kisiasa FCC na CASH, baada ya rais Etienne Tshisekedi kuvunja muungano huo Jumapili Desemba 6.

*RFI*

# Ureno kuisaidia Msumbiji kukabiliana na wanamgambo

**Cabo Delgado, MSUMBIJI**

URENO imejitolea kuisaidia Msumbiji kupanga mkakati na kuiwezesha jeshi la nchi hiyo, kukabiliana na wanamgambo wa Kiislamu wanaotishia usalama katika mkoa wa kaskazini wa Cabo Delgado wenye utajiri wa gesi.

Mwezi uliopita wanamgambo waligeuza uwanja wa michezo kuwa "kichinjio", ambako walikata watu vichwa na miili, kwa mujibu wa ripoti.

Waziri wa Ulinzi wa Ureno, Joao Gomes Cravinho, alisema kundi la wanajeshi wa nchi hiyo, kuanzia mwezi ujao litaanza kufanya kazi na wenzao wa Msumbiji.

Wiki iliyopita, Gomes Cravinho alikamilisha ziara ya kikazi ya siku tatu katika nchi hiyo ya Kusini mwa Afrika.

Alisema Ureno, ambayo itakuwa rais wa Muungano wa Ulaya kuanzia mwaka 2021, itaunga mkono ombi la Msumbiji la kupewa msaada ambalo tayari limewasilishwa Brussels.

Ghasia katika mkoa wa Cabo Delgado umesababisha mzozo wa kibinadamu, huku zaidi ya watu 2,000 kuuawa na wengine 560,000 kurudishwa kwao.

*BBC*




# MESSI

## KUPUNGUZIWA MSHAHARA AKIBAKI BARCA

**BAECELONA, Hispania**

LIONEL Messi ataondoka Barcelona kama hatakubali kukatwa mshahara, kwa mujibu wa mgombea urais wa klabu hiyo, Emili Rousaud.

Majaliwa ya Messi yamebaki kuwa majadala muhimu kwa miamba hao wa LaLiga kutokana na nyota huyo kuwasilisha maombi ya kutaka kuondoka baada ya kuwa na msimu mbaya 2019-2020.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, alikuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na miamba wa Ligi Kuu England, Manchester City kabla ya kuamua kubaki nchini Hispania, ingawa sasa anahusishwa na mabingwa wa Ligue 1, Paris Saint-Germain na Inter Milan.

Rousaud, ambaye anawania urais katika uchaguzi utakaofanyika Januari 24 baada ya kujiuzulu kwa Josep Maria Bartomeu Oktoba, amezungumzia kuhusu majaliwa ya Messi.

"Tutakaa chini na Messi na kumuomba apunguziwe mshahara wake," alisema Rousaud akiiambia ARA.

"Kwa sasa namna mambo yalivyo, ni jambo gumu kuendelea na mshahara uleule.

"Tutamuomba kujitolewa. Kama hakutakuwa na makubaliano, hivyo Messi ataondoka."

Rousaud aliongeza: "Messi ameandika historia ya kuvutia kwa klabu hii. Tunatakiwa kuwaheshimu magwiji wetu, lakini ukweli lazima usemwe.

"Naamini mambo yanatakiwa kusema kama yalivyo. Hatuweza kuwadanganya wajumbe wetu. Tutafanya kila jitihada za kuhakikisha anabaki, lakini mara zote maslahi ya klabu yatapewa kipaumbele."

Messi alifunga bao pekee kwa kikosi cha Ronald Koeman wakati kikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Levante kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, Jumapili.

## DYBALA ACHUKIZWA UVUMI WA MKATABA

**TURIN, Italia**

PAULO Dybala hafurahishwii na uvumi unaoendelea kuhusu majaliwa yake Juventus, akidai kwamba unamgombanisha na mashabiki.

Dybala alianza kuifungia Juventus kwenye mchezo wake wa saba wa Serie A msimu huu katika ushindi wa 3-1 dhidi ya Genoa Jumapili, huku mabao mawili ya penalti ya Cristiano Ronaldo yakikipa kikosi hicho ushindi, baada ya Stefano Sturaro kusawazisha.

Nyota wa zamani wa Palermo, Dybala mwenye umri wa miaka 27, amekuwa na mwanzo mgumu msimu huu, alisifiwa na kocha Andrea Pirlo baada ya mchezo huo.

Mkataba wa sasa wa Dybala pale Turin unamalizika msimu ujao, huku ripoti za hivi karibuni zikidai kwamba, mazungumzo kuhusu mkataba mpya yamesogezwa mbele kwa sababu ya nyota huyo wa Argentina kuwa na majeraha ya mara kwa mara.

Na uvumi huo sasa unafanya Dybala kuwa kweye wakati mgumu na mashabiki wake.

"Vitu vingi sana si vya kweli ambavyo vinasemwa sana kuhusu mkataba wangu," alisema Dybala akiiambia Sky Italia.

"Wakala wangu alikuwa Turin kwa muda mrefu na wala hakuitwa na klabu. Inanikatisha tamaa kusikia kwamba nataka kiasi kikubwa cha fedha.

"Litakuwa jambo zuri kama ukweli utasemwa, kwa sababu uvumi huu unaniweka katika taswira mbaya kwa mashabiki, hasa kutokana na mapenzi yote niliyopewa na Juventus."

## DORTMUND YAMTIMUA RASMI KOCHA FAVRE

**DORTMUND, Ujerumani**

KLABU ya Borussia Dortmund imemtimua kocha wake, Lucien Favre Jumapili huku msaidizi wake, Edin Terzic, akipandishwa kuchukua mikoba yake hadi mwishoni mwa msimu.

Kufukuzwa kwa Favre kumekuja baada ya timu hiyo kuchezea kichapo cha mabao 5-1 kutoka kwa Stuttgart Jumamosi.

Hicho kilikuwa kipigo cha tatu mfululizo kwa BVB nyumbani katika Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ikiwa ni kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2013-14, na kipigo kikubwa zaidi pale kwenye dimba la Westfalenstadion kwa kipindi cha muongo mmoja.

Baada ya mcheo huo, Dortmund wakatangaza kumtimua kocha huyo na Terzic akichukua majukumu yake.

Terzic kabla ya kuwa kocha, alizichezea klabu tofauti nne kwa kipindi cha miaka saba ya uchezaji wake, hakuna hata timu moja iliyokuwa daraja la juu zaidi ya madaraja ya chini.

Alianza kazi ya ukocha pale Dortmund baada ya miaka mitatu kuwa kwenye timu ndogo mwaka 2010, ambapo alikuwa kocha msaidizi wa timu ya vijana chini ya umri wa miaka 19.

Pia alikuwa akifanya kazi hapo wakati Jurgen Kloppa akiinoa timu hiyo.

## HABARI MICHEZO



# KLOPP
## ALIA KIWANGO KIBOVU LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp aliachwa akilalamika baada ya Liverpool kukosa nafasi ya kupaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa kulazimishwa sare na Fulham.

Wakati Tottenham ilicheza mapema na kuambulia pointi moja kwenye mchezo dhidi ya Crystal Palace, 'Wekundu' hao walijua kwamba kushinda pale katika dimba la Craven Cottage kungewafanya wapande kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

Hata hivyo, walishindwa kuupata ushindi dhidi ya vijana hao wa kocha Scott Parker, ambao walianza kwa kuongoza kupitia kwa Bobby Decordova-Reid na kuendelea kutengeneza nafasi nyingi za kufunga.

Liverpool ilipata sare hiyo baada ya Mohamed Salah kusawazishwa kwa mkwaju wa penalti.

Klopp baada ya mchezo huo aliiambia Sky Sports: "Hivyo hatukucheza vizuri. Kama tunataka kuamua... siwezi kuandika kitabu na kukirusha uwanjani na wao wakisome.

"Ninachotaka ni kwamba watatakiwa wao wenyewe kuelewa na kuanza mchezo. Mwanzo mzuri kwenye mchezo ni kitu kizuri, lakini kama hatuna mwanzo mzuri hivyo huwezi kuanza tena na tena.

"Tulihitaji nusu saa ya kuwa pamoja na kurudi mchezoni, ndio maana niliwafokea kidogo."

# MOURINHO AMTETEA LLORIS KWA SARE

**LONDON, England**

JOSE Mourinho amesema "golikipa bora kwenye Ligi Kuu ya England" Hugo Lloris si wa kulaumiwa kwa Crystal Palace kusawazisha dakika za mwisho baada ya Tottenham kulazimishwa sare ya 1-1, kwenye mchezo huo wa 'dabi' ya London.


Spurs walionekana kama wangepaa kileleni kwa pointi zaidi ya Liverpool baada ya golikipa wa Palace, Vicente Guaita kufanya makosa yaliyomzawadia bao la ufunguzi, Harry Kane pale kwenye dimba la Selhurst Park, Jumapili.

Hilo lilikuwa bao la 15 kwa Kane msimu huu na halikutosha kuwafanya Tottenham kuwafunga wapinzani wao wa jiji moja la London, baada ya Jeffrey Schlupp kusawazisha zikiwa zimebaki dakika 10 mchezo kumalizika.

Kocha wa Spurs, Mourinho alisema baada ya mchezo huo kwamba, hawezi kumnyooshea kidole Lloris, ambaye amemtaja kama kipa bora kwa Ligi Kuu England.

Alipoulizwa kama makosa ya Lloris yalichangia kwa bao la Schlupp, alisema: "Golikipa wangu ndiye kipa bora Ligi Kuu ya England, hivyo kamwe siwezi kumlaumu.

"Kama natakiwa kumlaumu mtu yeyote, basi tutajilaumu sisi wenyewe, halafu timu. Lakini si kwa golikipa kubeba lawama.



# RONALDO AFIKISHA MECHI 100 JUVE

**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo alisherehekea mechi yake ya 100 kwa Juventus kwa kufunga mabao mawili Jumapili kwenye ushindi wa 3-1 dhidi ya Genoa katika Ligi Kuu ya Italia na sasa yupo kwenye nafasi ya kufikisha mabao 1000.

Makosa ya walinzi yakawawezesha Juve kupata penalti mbili ndani ya dakika 12 za mwisho, na Ronaldo akazifunga zote kama alivyofanya dhidi ya Barcelona kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki iliyopita.

Ronaldo sasa amefikisha jumla ya mabao 77 aliyoifungia Juventus tangu alipotua klabuni hapo.

Si tu kwamba, Ronaldo alifikisha mechi yake ya 100 kwa Juve, pia alikuwa mchezaji wa kwanza Ulaya kufikisha mechi 400 za ushindi kwa ligi tano kubwa Ulaya katika karne hii.

Nyongeza, Ronaldo amefikisha mabao 31 kwa kalenda ya mwaka, na kumfanya kuwa mchezaji wa tatu wa Juve kufikisha idadi hiyo ya mabao tangu Omar Sivori mwaka 1961.


Akizungumza mara baada ya mchezo huo, Ronaldo aliiambia Sky Sport Italia: "Ilikuwa mechi ngumu, lakini nina furaha kwa mafanikio binafsi.

"Kule Barcelona tulishinda mchezo muhimu. Genoa wanacheza soka la kujilinda sana ilikuwa ni kazi ngumu kupata matokeo pale."

Halafu Ronaldo akaelezea namna alivyofurahia mafanikio hayo binafsi akiandika kwenye ukurasa wake wa Twitter: "Njia gani bora ya kusherehekea mechi ya 100 kwa Juventus, zaidi ya kufunga mabao mawili kwa timu?

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AFUNGUA MLANGO KUMRUDISHA OZIL KIKOSINI

●●●Hayupo kwenye kikosi kwa sasa, lakini chochote kinaweza kutokea Januari, tuna muda wa kutosha kuamua...

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amedokeza kwamba, kuna uwezekano wa kumrudisha kwenye kikosi cha 'Washika-budunduki' hao, Mesut Ozil.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani aliondolewa kwenye kikosi cha Arsenal kwenye ligi na mechi za kimataifa baada ya kufungwa kwa dirisha la usajili, na kumuacha yeye akiwa kwenye wakati mgumu pale katika dimba la Emirates.

Huku akiwa ameripotiwa kupata ofa za kutakiwa kuondoka klabuni hapo, Ozil aliamua kubaki licha ya kutopewa nafasi ya kuichezea timu hiyo kwenye mchezo wowote wa kimashindano.

Huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu wa 2020/21, ilionekana kama tayari amecheza mchezo wake wa mwisho akiwa na jezi ya Arsenal.

Hata hivyo, kauli ya hivi karibuni ya Arteta, Ozil anaweza kurudishwa kwenye kikosi cha Arsenal wakati wa kipindi cha dirisha dogo la usajili la Januari mwakani.

Akizungumza kuelekea mchezo wa kichapo wa Arsenal dhidi ya Burnley kwenye Ligi Kuu, Arteta alisema kuhusu Ozil; "Yeye (Mesut Ozil) hayupo kwenye kikosi kwa sasa. Nawaangalia zaidi wachezaji tulionao.

"Lakini chochote kinaweza kutokea Januari, tuna muda wa kutosha kuamua."

Ozil hajawahi kukichezea kikosi cha Arteta tangu Machi, na aliendelea kuachwa hadi alipotemwa kabisa kwenye kikosi hicho.

Ozil alitengeneza nafasi nyingi zaidi (146) kuliko mchezaji yeyote kwenye Ligi ya England wakati wa msimu wa 2015/16, akitoa pasi za mwisho 19.

## KWA UFUPI

**WAZAZI KUAMUA KWA MBAPPE**

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 21, amedokeza kwamba, nafasi ya yeye kuondoka Paris St-Germain inaweza kutegemea na maamuzi ya wazazi wake. ***(Copa 90)***

**JUVE YAMSIKILIZIA POGBA**

JUVENTUS ina matumaini Manchester United itamruhusu kiungo wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, kurudi pale Turin mwezi ujao kwa mkopo. (Mirror)

**BABA AMFUNGUKIA HALAAND**

BABA mzazi wa Erling Braut Haaland - mlinzi wa zamani wa Leeds, Alf-Inge - amesema straika huyo wa Norway mwenye umri wa miaka 20, kwa sasa ana furaha pale Borussia Dortmund, lakini anaweza kuondoka siku za usoni. (Tuttosport)

**EVERTON YAMTAKA DELE**

EVERTON ipo tayari kutoa ofa kwa kiungo, Dele Alli aondoke Tottenham Hotspur kwa kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 24 kwa mkopo Januari. ***(Star)***

**KHEDIRA ADOKEZA KUONDOKA**

KIUNGO wa Juventus, Sami Khedira, mwenye umri wa miaka 33, ambaye anataka kuondoka Januari, amethibitisha kwamba alikuwa na mawasiliano na kocha wa Everton, Carlo Ancelotti. ***(Bild)***

**ZIDANE AMKATAA ISCO**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema kiungo wa kimataifa wa Hispania, Isco hayupo kwenye mipango yake. Hata hivyo, kutopata nafasi ya kucheza kwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, katika klabu hiyo kunampa nafasi kubwa ya kuondoka Januari. ***(Marca)***

**RONDON AWANIWA WOLVES**

STRAIKA wa Venezuela, Salomon Rondon mwenye umri wa miaka 31, ambaye kwa sasa anaichezea klabu ya nchini China ya Dalian Pro, anahusishwa na Wolves baada ya kuumia kwa Raul Jimenez. ***(Sun)***

**PSG KUMSAJILI DEPAY**

PARIS St-Germain inaweza kumsajili straika wa Lyon na Uholanzi, Memphis Depay kipindi cha majira ya joto, lakini Barcelona wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa muda mrefu. ***(Le Parisien)***

**SPURS YAMTAKA DYBALA**

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo tayari kuilipa Juventus pauni milioni 63.6 kwa ajili ya kumsajili straika wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 27. ***(TodoFichajes)***

**PSG YAJITOSA KWA AOUAR**

KIUNGO wa Lyon, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 22, ambaye amekuwa akiwaniwa na Arsenal, pia anawaniwa na Paris St-Germain. ***(RMC)***

**SORINOLA AWANIWA ENGLAND**



KLABU za Ligi Kuu ya England, Leeds na West Ham ni miongoni mwa klabu nyingi zinazomuwania mlinzi wa MK Dons, Matthew Sorinola, mwenye umri wa miaka 19. ***(Teamtalk)***

HABARI MICHEZO

# MGUNDA SOKONI KUTAFUTA WAKUIBORESHA COASTAL

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kushuhudia kikosi chake kikilazimishwa sare tasa ya pili nyumbani, Kocha Mkuu wa Coastal Union ya Tanga, Juma Mgunda, amesema, hakuna namna lazima amulike wachezaji wa kukiimarisha kikosi chake katika dirisha dogo la usajili lililofunguliwa rasmi leo.

Juzi ikiwa katika Uwanja wake wa Mkwakwani jijini Tanga, Coastal ililazimishwa sare tasa dhidi ya Tanzania Prisons matokeo ambayo pia iliyapata Desemba 5, mwaka huu uwanjani hapo dhidi ya Mbeya City.

Sare hiyo ni ya tatu mfululizo kwa Coastal Union kwani kabla ya mechi hizo mbili za nyumbani, ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, hivyo kuifanya kushika nafasi 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 18 baada ya kushuka dimbani mara 15.

Na baada ya matokeo hayo ya juzi, Mgunda aliweka wazi kuwa ataingia sokoni katika dirisha hili kukiboresho kikosi chake ambacho msimu huu kimepunguzwa kasi kutokana na kuwapoteza baadhi ya nyota wake wakiwamo mabeki pacha, Bakari Mwamnyeto anayekipiga Yanga na Ibrahim Ame aliyetua Simba.

Kuondoka kwa mabeki hao wawili kuimeifanya Coastal kuwa miongoni mwa timu zenye safu dhaifu ya ulinzi, kwani hadi sasa ndiyo inayoongoza kwa kufungwa mengi (7-0) katika mchezo mmoja msimu huu, baada ya kukubali kipigo hicho dhidi ya Simba zilipokutana Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Lakini pia Coastal Union ni timu ya tatu hadi sasa kuruhusu mabao mengi (18) baada ya Mwadui FC ambayo imeruhusu nyavu zake kutingishwa mara 33 ikifuatiwa na JKT Tanzania iliyotobolewa mara 19.

"Lazima nifanyie maboresho safu yangu ya ulinzi na ushambuliaji kwenye dirisha dogo, hivyo mipango ikikamilika kila kitu kitawekwa wazi, kwa sasa tusubiri kwanza," alisema Mgunda.

## HESHIMA KIMATAIFA...



Wachezaji wa timu ya Combine ya Kasulu na Uvinza mkoani Kigoma pamoja na baadhi ya viongozi wao, wakisherehekea ubingwa wa Lake Tanganyika Cup baada ya kuutwa kwa kuifunga Academy ya Mkoa wa Ruyigi, Burundi kwa mabao 2-0, kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Nkurunzinza Peace Complex uliopo Mkoa wa Makamba nchini Burundi. **PICHA: PENDO THOMAS**

# Kocha Mwadui amwaga 'upupu' akiachia ngazi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, ameianika klabu hiyo baada ya kutangaza kumwaga manyanga ya kuendelea kuinoa, ikiwa ni siku moja tangu aiongoze kupokea kipigo cha mabao 5-0 dhidi ya Yanga.

Jumamosi Mwadui ikiwa katika uwanja wake wa nyumbani mkoani Shinyanga, ilikubali kipigo cha mabao 5-0 dhidi ya Yanga na siku iliyofuata, Adam alitangaza kuachia ngazi.

Hatua hiyo ilitokana na uongozi kutofurahishwa si tu kwa matokeo hayo, bali pia mwenendo mzima wa Mwadui FC wa kusuasua katika ushiriki wake wa Ligi Kuu msimu huu.

Lakini Adam amesema ameamua kuachana na timu hiyo kutokana na kubebeshwa lawama za timu kufanya vibaya huku akiambiwa ni matokeo ya yeye kusajili wachezaji ambao hawana uwezo.

"Nimeambiwa kuwa nimesajili wachezaji ambao hawana uwezo, ndiyo maana napoteza mechi. Lakini mimi nilisajili baada ya kuona siku zinakwenda na hakuna pesa za kusajili. Na timu hii haijasajiliwa hata na shilingi 10,000, nilichofanya ni kuita wachezaji kwenye majaribio, tukapata tuliowapata, tunashukuru Mungu ndiyo wametufikisha hapa.

"Kocha unaweza kulaumiwa kama mahitaji yote kwa timu yanatekelezwa, hapa nilipo tangu msimu umeanza wachezaji wamelipwa mshahara wa mwezi mmoja tu na hata vifaa vya mazoezi ni tabu, timu nzima ina mipira sita wakati unatakiwa uwe na angalau mipira 40," alisema.

Alipoulizwa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Nurdin Suleiman, alizunguka swali hilo akieleza si kweli kama kocha huyo hajapewa pesa ya usajili.

"Sidhani kama alikosa pesa ya usajili na suala kama hili ni letu kati yeye na sisi, hivi vipo ndani ya wajumbe," alisema Nurdin.

Kuhusu kulipwa mshahara wa mwezi mmoja tu mpaka sasa, mwenyekiti huyo alisema kuwa hana uhakika, lakini atakapokabidhiwa rasmi ofisi na makabrasha yote, ndipo anaweza kujua kama hilo lipo au la.

Mwadui FC imekuwa ni kama ada kwao kupachikwa idadi kubwa ya mabao kwani, ilichapwa mabao 6-1 dhidi ya JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Mwadui Complex, Oktoba 25, mwaka huu, na Oktoba 30, ikabugizwa 5-0 dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Kabla ya mechi ya jana kati ya Mtibwa dhidi ya Ihefu inayoshika mkia kwa pointi saba, Mwadui ilikuwa inashika nafasi ya 17 ikiwa na pointi 10.

# Mtifuano Daraja la Kwanza Z'bar Ijumaa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR.**

LIGI Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inatarajiwa kuanza kutimua vumbi Ijumaa wiki hii, mchezo wa ufunguzi ukizikutanisha timu ya Taifa Jang'ombe dhidi ya Ngome katika Uwanja wa Amaan.

Ligi hiyo msimu huu itachezwa katika viwanja sita vikiwamo viwanja vya nje ya mji wa Zanzibar, tofauti na msimu uliopita ambapo ilichezwa katika viwanja viwili vya ndani ya mji wa Zanzibar.

Viwanja ambavyo ligi hiyo itatimua vumbi ni Amaan, Mau, Mchangani, Bungi, Kinyasini na Uwanja wa Kichakanyuki.

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Kassim Mohmed, alisema maandalizi yote ya kuelekea ligi hiyo yamekamilika hususan viwanja ambavyo vitatumika kuchezewa ligi hiyo vilivyopo nje ya mji wa Zanzibar, ambavyo ameeleza vinaridhisha baada ya bodi hiyo kuvifanyia marekebisho.

"Timu tayari zimeshapewa ratiba, kinachofuata ni kuhakikisha wanafuata ratiba za mechi zao, msimu huu, ambazo zote zitachezwa katika viwanja vya nyumbani na ugenini, hivyo kwa wale ambao viwanja vyao vipo nje ya mji, wahakikishe usalama unakuwapo na bodi ya ligi pamoja na kamati ya mashindano italizingatia hilo," alisema

# Malale: Mastarika tatizo Polisi Tanzania

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI ikiifuata Mwadui FC baada ya kutoka kulazimishwa sare tasa nyumbani dhidi ya Ruvu Shooting, timu ya Polisi Tanzania imeendelea kulia na safu yake ya ushambuliaji kushindwa kuzibadili nafasi za mwisho wanazozitengeneza kuwa magoli.

Ikiwa katika Uwanja wake wa Ushirika mjini Moshi, Polisi Tanzania ililazimishwa sare tasa na Ruvu Shooting Jumamosi kwenye mechi ambayo benchi la ufundi linalalamikia washambuliaji wake kuendelea kushindwa kutumia vema nafasi wanazotengenezewa.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka Moshi mkoani Kilimanjaro, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Malale Hamsini, alisema suala hilo linamchanganya kwa kiasi kikubwa.

"Safu yangu ya ushambuliaji ina upungufu, mara nyingi tunapokuwa tunacheza wanapata nafasi nyingi za wazi tatizo limekuwa kushindwa kuzitumia," alisema Malale.

Alisema anachokifanya kwa sasa ni kuhakikisha tatizo hilo linamalizika ili lisiwape shida kwenye michezo ya mbeleni hususan dhidi ya Mwadui Ijumaa, ambayo imetoka kuchezea mabao 5-0 nyumbani dhidi ya Yanga.

"Ninaendelea kufanyia kazi upungufu niliyouona katika michezo ambayo tumeicheza pamoja na ule wa juzi ambao tumecheza na timu ya Ruvu Shooting," alisema.

Michezo
Jumanne Desemba 15, 2020
Nipashe




## ARTETA AFUNGUA MLANGO KUMRUDISHA OZIL

HABARI UK 22

WAYA...




Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi (Jezi Na. 10) , akiifungia timu yake bao pekee dakika ya 76, wakati ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Levante, katika mechi ya Ligi Kuu Hispania iliyopigwa Uwanja wa Camp Nou juzi. **HABARI UK. 20**

# UEFA YAMRUDISHA NEYMAR BARCELONA

## ●●●Ronaldo arejeshwa Ureno, Klopp Ujerumani, huko Ligi ya Europa Arsenal, United kazi ipo...

**Nyon, Uswisi**

MABINGWA wa LaLiga, Barcelona na wa Ligue 1, Paris Saint-Germain wataingia tena vitani kukumbushia hatua ya 16-Bora ya Ligi ya Mabingwa msimu 2016-17 baada ya miamba hiyo kupangwa tena kukutana katika hatua hiyo msimu huu kwenye droo iliyochezeshwa jijini Nyon, Uswisi jana.

Barca inakumbukwa kwa kuwa timu ya kwanza kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kupindua matokeo ya mechi ya awali baada ya kulala kwa mabao 4-0 ugenini dhidi ya PSG na kisha kushinda nyumbani 6-1 katika mechi ya marudiano ya hatua hiyo ya 16-Bora msimu wa 2016-17.

Neymar alicheka na nyavu mara mbili na kutoa pasi mbili za mabao kwa Sergi Roberto wakati Barca ikiibuka na ushindi, lakini uwezekano wa kuivaa klabu yake hiyo ya zamani akiwa na PSG unaweza kuwa shakani kutokana na nyota huyo wa Brazil kupata majeraha makubwa ya kifundo cha mguu ('ankle') wakati wakichezea kichapo cha bao 1-0 nyumbani dhidi ya Lyon juzi.

Barca pia iliichapa PSG katika hatua ya robo fainali katika safari yao ya kutwaa mataji matatu msimu wa 2014-15 na katika hatua ya robo fainali msimu wa 2012-13.

PSG ilifika fainali katika michuano hiyo ambayo ilichelewa kumalizika msimu uliopita kutokana na kuibuka kwa janga la virusi vya corona, na mabingwa watetezi Bayern sasa watajiandaa kuvaana na wakali wa Serie A, Lazio ikiwa ni kwa mara ya kwanza kwenye michuano hiyo ya Ulaya.

Jurgen Klopp akiwa na mabingwa wa michuano hiyo msimu wa 2018-19, Liverpool, amerejeshwa Ujerumani, kuivaa RB Leipzig, wakati kukiwa na sehemu nyingine ya timu ya Bundesliga itakayovaana na miamba ya Ligi Kuu England, Borussia Monchengladbach dhidi ya Manchester City - ambazo zilikutana hatua ya makundi msimu wa 2015-16 na 2016-17.

Mbio za 'Wekundu wa Anfield' hao kutetea ubingwa wao zilihitimishwa na Atletico Madrid msimu uliopita na vinara hao wa LaLiga sasa wana malengo ya kupata mafanikio zaidi msimu huu watakapowavaa miamba mingine ya Ligi Kuu England, Chelsea, inayonolewa na Frank Lampard ambaye alikuwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo wakati kikitwaa ubingwa huo mwaka 2012.

Real Madrid, ambao wanashikilia rekodi ya kutwaa taji hilo mara 13, watakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Atalanta, wakati kocha Andrea Pirlo na Juventus yake watamrejesha Cristiano Ronaldo Ureno kwenda waivaa Porto, huku Sevilla wakiangukia mikononi mwa Borussia Dortmund inayoongozwa na 'mashine' ya mabao, Erling Haaland.

Mechi za kwanza za hatua hiyo ya 16-Bora zitapigwa kati ya Februari 16 na 17, na zingine 23 na 24, wakati marudiano yakiwa Machi 9 na 10, pamoja na 16 na 17.

**UEFA**

| | |
|---|---|
| Borussia Monchengladbach v Man City | |
| Lazio | v Bayern Munich |
| Atletico Madrid | v Chelsea |
| RB Leipzig | v Liverpool |
| Porto | v Juventus |
| Barcelona | v Paris Saint-Germain |
| Sevilla | v Borussia Dortmund |

**LIGI YA EUROPA**

Kwa upande wa michuano ya Ligi ya Europa hatua ya 32, Manchester United itaanzia nyumbani dhidi ya Real Sociedad, Arsenal ikianzia ugenini dhidi ya Benfica, mechi za kwanza zikipigwa Februari 18, mwakani na marudiano wiki inayofuata, huku Spurs nayo ikianzia ugenini dhidi ya Wolfsberger ya Ujerumani.

Mechi nyingine zitakuwa kati Dynamo Kiev na Club Brugge, Red Star Belgrade dhidi ya Milan, Royal Antwerp vs Rangers, Slavia Prague vs Leicester City, Salzburg vs Villarreal na Braga vs Roma, Krasnodar vs Dinamo Zagreb na Young Boys dhidi ya Bayer

## SIMBA SASA YALIA MAREFA KUWAFINYA

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kukiri timu yake kutokucheza soka lao la kuvutia lililozoeleka wakati wakiibuka na ushindi finyu wa bao 1-0 dhidi ya Mbeya City juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amelalamikia kitendo cha mwamuzi wa mchezo huo, Martin Saanya, kushindwa kuwalinda wachezaji wake na kuwaacha wakichezewa rafu zisizo za kiungwana.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Sokoine, Simba ilishindwa kuonyesha soka lake la kuvuti, lakini Sven alisema kikubwa ni pointi tatu ambazo zinawawezesha kuendelea kuwa kwenye mbio za ubingwa wakati huu wakijiandaa pia na mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika kuwania kufuzu hatua ya makubdi ya michuano hiyo.

Sven alisema mwamuzi Saanya, alishindwa kuwalinda wachezaji wake, jambo ambalo liliwafanya kushindwa kuonyesha ufanisi wao mchezoni.

"Refa aliruhusu wachezaji wangu kuchezewa rafu nyingi ila kama timu tulicheza vizuri na si suala la mchezaji mmoja mmoja," alisema.

Malalamiko hayo ya Sven pia yalitolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, ambaye baada ya mechi hiyo kumalizika, aliandika kwenye mtandao wake wa kijamii kuwapongeza wachezaji wake, lakini akilalamika kwa mwamuzi kutokana na uchezeshaji wake.

"Mwenendo wa waamuzi Tanzania una changamoto sana. Mchezo umekuwa wa kufedhehesha kwa timu yetu. Wamecheza vizuri ukiangalia mazingira ya mchezo."

Lakini pia Barbara alinukuliwa akisema: "Tumechoka 'this is too much', TFF sasa iwaangalie waamuzi si kwa mchezo huu tu hata iliyopita."

Lakini kwa upande wa Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, alisema kikosi chake kilikosa mmaliziaji, pia akidai ni wakati wa kufanya mabadiliko kwa baadhi ya wachezaji ndani ya timu hiyo kipindi hiki cha dirisha dogo.

"Nimepoteza, matokeo si mazuri, lakini tumecheza vizuri. Tatizo tunaingia kwenye eneo la hatari, nafasi zinapatikana lakini hatuwezi kuweka mpira ndani ya nyavu," alisema kocha huyo ambaye ni mechi yake ya kwanza kusimama kama kocha mkuu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002